# KUCHUNGUZA TASWIRA KATIKA NYIMBO ZA TAARAB ZA KIMAHABA ZA KHADIJA KOPA

**SAUDA RASHID MASSOUD**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI (M.A KISWAHILI) KATIKA IDARA YA LUGHA NA TAALUMA ZA FASIHI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2022**

## ITHIBATI YA MSIMAMIZI

Aliyesaini hapo chini, anathibitisha kwamba, ameisoma tasnifu inayoitwa; ***Kuchunguza Taswira katika Nyimbo za Taarab za Kimahaba za Khadija Kopa*** na amependekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kwa ajili kutunukiwa Shahada ya Uzamili ya Kiswahili katika Idara ya Lugha na Taaluma za Fasihi ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

…………………………………….

Dkt. Felistas Richard Mahonge

(Msimamizi)

Tarehe …………………………

## IKIRARI

Mimi, **Sauda Rashid Massoud**, nathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu halisi na kwamba haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote, kwa ajili ya masomo ya Uzamili.

**Saini ………………………………………..…………….**

**Tarehe……………………………………………………**

## HAKI MILIKI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuzalisha, kunakili, wala kusambaza sehemu yoyote ya tasnifu hii, kwa namna yoyote, bila ya ruhusa ya mtafiti ama Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

## TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa mama yangu kipenzi BiSalma Abdalla Ali na baba yangu mpendwa Bwana Rashid Massoud Rashid wao ndio walionilea na kunikuza kielimu hadi leo nimefikia kiwango hiki cha elimu Pia, baba na mama ni walimu wangu kuanzia nilipozaliwa hadi leo. Namuomba Mwenyezi Mungu awape umri mrefu hapa duniani na maisha ya baadae akawaingize peponi. Amin.

## SHUKURANI

Mwanzo kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniumba, kunikuza, kunipa afya, akili na fahamu na kutia neno hadi kuikamilisha kazi hii muhimu katika maisha yangu. Maamuzi yake ya kila kitu kukiambia “kuwa” ndio “kikawa” ndiyo yaliyopelekea kukamilika kwa tasnifu hii.

Pili, napenda kumshukuru kwa dhati msimamizi wangu wa utafiti huu Dkt. Felistas Richard Mahonge ambaye amejaa busara, hekima na ucheshi katika kutoa maelekezo ya kazi hii hadi pale ilipokamilika. Juhudi zake za kipekee sitazisahau maishani mwangu na namuahidi kwamba yupo rohoni mwangu hadi nitakapofumba jicho kurudi kwa Mwenyezi Mungu.

Tatu, namshukuru mama yangu Bi Salma Abdalla Ali na baba yangu Rashid Massud Rashid pamoja na mume wangu kipenzi Bwana Amour Moh’d Salim kwa kunisaidia na kunitia moyo hadi kukamilika kwa utafiti huu. Aidha, ninamshukuru mwanangu mpenziMaliyha Amour Moh’d kwa uvumilivu wake katika kipindi chote cha masomo yangu.Bila kuwasahau ndugu zangu wote ambao waliniunga mkono kwa kunilelea mtoto wangu wakati nikiwa masomoni.

Nne, nawashukuru wahadhiri wangu wote wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Hawa ni wengi. Hivyo nitawataja lakini naamini kwamba si hao tu waliosaidia katika ngazi hii ya elimu. Baadhi ya wachache ni Dk.Omar Maguo, Dk Hilda Pembe, Dk.Zelda Elisifa, Mw.Bakar Kombo, Mw.Sharifu Faki na wengineo.

Tano, ninawashukuru kwa dhati wanafunzi wenzangu wote wa fani ya Fasihi ya Kiswahili. Ushirikiano na msaada wao kwangu ulisadifu sana katika kufanikisha masomo yangu.Hapa nawataja kwa uchache,Bi Fatma Rashid Massoud,Bi Kauthar

Is-haka Mzee ,Bi Maymuna Ali Haji na wengineo nawashukuru kwa msaada wao mkubwa wa namna ya kuikamilisha kazi hii kivitendo.

## IKISIRI

Tasnifu hii inahusu **Kuchunguza Taswira katika Nyimbo za Taarab za Kimahaba za Khadija Kopa.** Utafiti ulilenga kuzibainisha taswira zinazotumiwa na Khadija Kopa katika nyimbo za mahaba za Khadija Kopa, kubainisha miktadha ya matumizi ya taswira katika nyimbo za taarab za mahaba za Khadija Kopa. Na kuchunguza athari za taswira hizo kwa jamii. Mbinu iliyotumika kupata data ni usomaji makini. Mtafiti alizisikiliza huku akizinukuu nyimbo za taarab 21 za Khadija Kopa katika mtandao wa “You Tube” na kuchagua nyimbo 5 ambazo ndizo alizoziwasilisha na kuzifanyia uchambuzi kwa njia ya maelezo na majadwali. Nyimbo hizo ni *Niliwaze*, *Nimemridhi, Mwanamke Mambo*, *I Love You* na *Full Stop*. Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni nadharia ya Simiotiki. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa nyimbo za mahaba za Khadija Kopa zinatumia taswira za za kizuolojia, taswira za botania, taswira za kiastromia, taswira za kijiolojia, taswira ya kiteolojia na taswira za vitu vya kawaida. Pia, matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa miktadha inayosababisha ubunifu wa taswira katika nyimbo za Khadija Kopa ni miktadha ya mapenzi, miktadha ya utamaduni, miktadha ya utandawazi, miktadha ya imani na miktadha ya kifasihi. Kwa upande wa athari za taswira hizo kwa jamii, utafiti umebaini kuwa kuna athari chanya na hasi. Athari chanya ni pamoja na kukuza lugha, kuendeleza utamaduni, kukuza fasihi, kutambulisha na kuifunza jamii. Kwa upande wa athari hasi ni kuhamasisha ngono holela, kuendeleza mawazo ya kumfanya mwanamke kuwa chombo cha starehe dhidi ya mwanamme, kutumia lugha ya matusi na kuchochea migogoro. Mwisho utafiti umependekeza kuwa ipo nafasi ya kufanya tafiti nyengine katika nyimbo za taarab zikiwa na malengo tofauti na utafiti huu kama vile kuchunguza majigambo ya watrib wa nyimbo za taarab hasa za wanawake akiwemo Khadija Kopa.

**Maneno Makuu:** *Taarab, Majigambo, Nyimbo*

# YALIYOMO

ITHIBATI YA MSIMAMIZI ........ ii
IKIRARI ........ iii
HAKI MILIKI ........ iv
TABARUKU ........ v
SHUKURANI ........ vi
IKISIRI ........ viii
YALIYOMO ........ ix
ORODHA YA MAJADWALI NA VIAMBATANISHO ........ xiv

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI KWA UJUMLA ........ 1**

1.0 Utangulizi ........ 1
1.1 Usuli wa Mada ........ 1
1.2 Khadija Kopa na Kazi zake za Kifasihi Katika Kipera cha Nyimbo ........ 3
1.3 Tatizo la Utafiti ........ 4
1.4 Malengo ya Utafiti ........ 5
1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti ........ 5
1.4.2 Madhumuni Mahasusi ........ 6
1.5 Maswali ya Utafiti ........ 6
1.6 Umuhimu wa Utafiti ........ 6
1.7 Mipaka ya Utafiti ........ 7
1.8 Changamoto za Utafiti na Utatuzi wa Changamoto ........ 7
1.9 Mpangilio wa Tasnifu ........ 8

**SURAYA PILI: UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MIKABALA YA KINADHARIA ..... 9**

2.1 Utangulizi ..... 9

2.2 Ufafanuzi wa Dhana ..... 9

2.2.1 Maana ya Nyimbo ..... 9

2.2.2 Nyimbo za Mahaba ..... 11

2.2.3 Dhana ya Taswira ..... 12

2.2.4 Mgawanyo wa Taswira ..... 13

2.5 Tafiti Kuhusu Nyimbo za Taarab ..... 17

2.6 Pengo la Utafiti ..... 21

2.7 Mkabala Wa Kinadharia ..... 22

2.7.1 Nadharia ya Simiotiki ..... 22

2.7.1.1 Misimbo ya Nadharia ya Simiotiki ..... 23

2.8 Hitimisho ..... 25

**SEHEMU YA TATU: MBINU ZA UTAFITI ..... 26**

3.1 Utangulizi ..... 26

3.2 Eneo la Utafiti ..... 26

3.3 Usanifu wa Utafiti ..... 26

3.4 Walengwa wa Utafiti ..... 27

3.5 Sampuli na Usampulishaji ..... 27

3.5.1 Sampuli ..... 27

3.5.2 Usampulishaji ..... 28

3.5.2.1 Mbinu ya Uteuzi wa Madhumuni Maalumu ..... 28

3.6 Data za Utafiti ........ 29
3.6.1 Data za Msingi ........ 29
3.6.2 Data za Upili ........ 29
3.7 Mbinu za Kukusanya Data ........ 30
3.7.1 Mbinu ya Upitiaji wa Nyaraka andishi ........ 30
3.8 Uchambuzi wa Data ........ 31
3.9 Hitimisho ........ 31

**SURA YA NNE: UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI ........ 32**

4.0 Utangulizi ........ 32
4.1 Taswira katika Nyimbo za Taarab za Khadija Kopa ........ 32
4.2 Taswira za Kizuolojia ........ 32
4.2.1 Taswira za Botania ........ 37
4.2.2 Taswira za Kiastromia ........ 39
4.2.3 Taswira za Kijiolojia ........ 41
4.2.4 Taswira za Kiteolojia ........ 42
4.2.5 Taswira za Vitu vya Kawaida ........ 45
4.3 Miktadha ya Matumizi ya Taswira katika Nyimbo za Taarabu za Khadija Kopa ........ 55
4.3.1 Miktadha ya Mapenzi ........ 55
4.3.3 Miktadha ya Utandawazi ........ 62
4.3.4 Miktadha ya Imani ........ 64
4.3.5 Miktadha ya Kifasihi ........ 66

4.4 Athari za Matumizi ya Taswira Katika Nyimbo za Khadija Kopa ................ 69
4.4.1 Athari Chanya za Matumizi ya Taswira katika Nyimbo za Khadija Kopa .... 69
4.4.1.1 Kukuza Lugha ........................................................................................ 69
4.4.1.2 Kuendeleza Utamaduni ........................................................................ 71
4.4.1.3 Kukuza Fasihi ........................................................................................ 72
4.4.1.4 Kutambulisha Uwezo wa Mungu ........................................................ 75
4.4.1.5 Kuifunza Jamii ...................................................................................... 76
4.4.2 Athari Hasi za Taswira katika Nyimbo za Taarab za Khadija Kopa ............. 78
4.4.2.1 Kuhamasisha Ngono Holela ................................................................ 78
4.4.2.2 Kuendeleza Mwanamke Kuwa Chombo cha Starehe cha Mwanamme ........ 79
4.4.2.3 Matumizi ya lugha ya Matusi ............................................................... 80
4.4.2.4 Kuchochea Migogoro ........................................................................... 81
4.5 Hitimisho ........................................................................................................ 82

**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .......... 83**

5.1 Utangulizi ........................................................................................................ 83
5.2 Muhtasari wa Tasnifu ..................................................................................... 83
5.3 Matokeo ya Utafiti .......................................................................................... 85
5.3.1 Lengo Mahususi la Kwanza ........................................................................ 85
5.3.2 Lengo Mahsusi la Pili ................................................................................. 85
5.3.3 Lengo Mahsusi la Tatu ................................................................................ 86
5.4 Hitimisho ........................................................................................................ 86
5.5 Mapendekezo .................................................................................................. 86
5.5.1 Mapendekezo kwa Watafiti Wengine .......................................................... 87

5.5.2 Mapendekezo kwa Wasanii wa Nyimbo za Taarab ........................................ 87

5.5.3 Mapendekezo kwa Jamii ..................................................................................... 87

**MAREJELEO…. .......................................................................................... 88**

**KIAMBATANISHO ........................................................................................ 93**

## ORODHA YA MAJADWALI NA VIAMBATANISHO

Jadwali Na. 4.1.1 Taswira za Kizuolojia Katika Nyimbo za Taarab za Khadija Kopa ............ 33

Jadwali Na. 4.1.2 Taswira za Botania katika Nyimbo za Khadija Kopa ............ 37

Jadwali Na. 4.1. 3 Taswira za Kiastromia za Khadija Kopa............ 39

Jadwali Na. 4.1.4 Taswira za Kijiolojia katika Nyimbo za Khadija Kopa ............ 41

Jadwali Na. 4.1.5 Taswira za Kiteolojia katika Nyimbo za Khadija Kopa ............ 42

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI KWA UJUMLA

## 1.0 Utangulizi

Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza taswira katika nyimbo za taarabu za mahaba za Khadija Kopa. Utafiti umeangalia aina za taswira zinazotumiwa na miktadha inayosababisha mtunzi kutumia taswira hizo na athari zake kwa jamii. Sura hii inabainisha vipengele muhimu vya kiutangulizi ambavyo ni pamoja na mada ya utafiti, usuli wa mada ya utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti na maswali ya utafiti. Pia, sehemu hii inaeleza umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti huu na muundo wa tasnifu.

## 1.1 Usuli wa Mada

Utafiti huu unahusu kuchunguza taswira katika nyimbo za taarab za kimahaba za Khadija Kopa. Nyimbo za taarab ni nyimbo ambazo huimbwa katika ngoma ya taarab. Njogu na Wafula (1993) wanaeleza kwamba "taarab" ni neno lenye asili ya Kiarab lenye maana ya furaha, kusheherekea, karamu, kuimba na kupiga muziki. Wanaendelea kueleza kwamba mbali na neno lenyewe kuwa la kigeni hata ngoma na muziki wenyewe ni wa kigeni. Hivyo wataalamu wengi wanadai kwamba hii si fasihi simulizi yenye chimbuko lake hapa Afrika. Inasemekana taarab hujitenga na ngoma nyengine kutokana na ala zinazotumiwa na kwa nidhamu ya ngoma hiyo.

Njogu na Wafula (1993) wanaendelea kueleza kuwa taarab ni ngoma ya nyimbo na vinanda. Kinyume na ngoma zingine tuzijuazo katika ngoma ya taarab hakuna kucheza. Wapiga ngoma na vinanda hujikusanya pahali pamoja na wasikilizaji huwakabili ama huwazingira. Ngoma ya taarabu inapoanza wasikilizaji huwa kimya

na jukumu lao huwa ni kutega masikio tu kwa milio ya vinanda na sauti ya maneno ya mtiribu ya ngoma wenyewe. Maelezo haya yanayoelezwa hapa yanajikita zaidi kufafanua sifa ya taarab ya kabla ya taarab ya kisasa. Kwa uzoefu wa mtafiti ni kwamba leo hii taarab imekuwa ikipigwa huku watazamaji pamoja na waimbaji wakicheza kwa pamoja na hata kuimba nyimbo hiyo katika baadhi ya mikarara yake.

Kihistoria nyimbo za taarab ziliingia katika upwa wa Pwani ya Afrika Mashariki miongo kadhaa iliyopita. Kama aelezavyo Saleh (1980) kwamba taarab iliingizwa katika jamii ya Uswahilini kati ya miaka ya 1870-1888 wakati wa Sultan Barghash bin Said. Anaendelea kueleza kwamba inasemekana Barghash alikuwa mpenda muziki na alikuwa anaburudishwa kwa kutumia ngoma ya taarabu.

Nyimbo za taarab kama zilivyokuwa tanzu nyengine za fasihi zenye mielekeo ya urasimi mkongwe hapo mwanzo zililenga kuwasifu watu wa tabaka la juu. Mawazo haya yanaungwa mkono na Njogu na Wafula (1993) ambao wanaeleza kuwa nyimbo za taarab kimaudhui zilikuwa zikisifu na kumtukuza Sultani na dhuria yake. Wakati mwengine ngoma ya taarabu ilisifu na kukomaza mapenzi ya jumuiya ya kifalme. Pia, zilitumika kuwaburudisha na kuwachekesha wakubwa. Hivyo wachezaji wa taarabu walikuwa wanaajiriwa katika nyumba za wafalme kuwastarehesha na vinanda vyao.

Kwa upande wa matumizi ya lugha Njogu na Wafula (1993) na Simiyu (2011) wanaeleza kwamba nyimbo za taarab hutumia Kiswahili cha hali ya juu. Kama inavyobainika katika muundo wa taarab, kuna matumizi ya mtindo wa lugha ya kishairi, hasa kwa vile kunakuwa na uzingativu wa kaida za ushairi wa Kiswahili. Urari wa vina na mizani na arudhi nyengine za ushairi wa Kiswahili ni baadhi ya

mambo yanayojidhihirisha katika nyimbo za taarab. Aidha, matumizi ya lugha ya kiishara na mafumbo hujidhihirisha kutokana na kutumika katika arudhi ya ushairi. Matumizi haya ya lugha kiishara na mafumbo hufanya nyimbo za taarabu kuwa ngumu kueleweka. Ingawa katika mjadala huu Njogu na Wafula hawagusii lugha ya taswira, lakini kipengele hiki kimekuwa ni uti wa mgongo wa nyimbo za taarab.

Hivi leo taarabu imechukuwa mabadiliko makubwa katika kipengele cha utendaji, fani na maudhui yake. Wakati wa kuimbwa nyimbo hizo hadhira hushiriki katika kuimba ama kucheza pamoja na muimbaji ama waimbaji. Aidha, maudhui ya taarabu kwa sasa yanasawiri masuala ya kijamii kama vile siasa, uchumi, utamaduni na mapenzi. Mabadiliko haya yanachochewa na miktadha mbalimbali kama miktadha hiyo inavyoelezwa na Khamisi (2017) ambaye katika utafiti wake wenye mada "Mabadiliko katika Nyimbo za Taarab na Uwasilishaji Wake Kulingana na Wakati" alibaini kuwa vipindi mbalimbali vya kihistoria kama vile kipindi cha utawala wa Sultani, kipindi cha harakati za mapinduzi na uhuru, baada ya mapindiuzi hadi sasa ndivyo vilivyoathiri moja kwa moja nyimbo za taarab.

## 1.2 Khadija Kopa na Kazi zake za Kifasihi Katika Kipera cha Nyimbo

Khadija Kopa ni mmoja wa waimbaji nguli wa nyimbo za taarabu zenye kujaa mahaba. Nyongesa (2013) anasema kuwa Khadija Kopa ambaye hujulikana pia kwa jina la utani kama Malkia wa mipasho au Sauti ya chiriku alizaliwa mwaka 1963 katika Visiwa vya Zanzibar akiwa ni mtoto wa pekee katika familia ya Kopa. Ameolewa na ana watoto wanne na wajukuu wawili. Kwa bahati mbaya mwanawe mmoja, Omar Kopa, ambaye pia alikuwa muimbaji wa kutajika alifariki. Mbali na muziki Khadija Kopa ni mama wa nyumbani, mfanyabiashara na mwanaharakati za

kisiasa nchini Tanzania. Kwa mara ya kwanza alijiunga kuimba katika Culture Musical Club ambapo alipelekwa na babu yake baada ya kuona kipaji alichokuwa nacho. Ingawa kabla ya hapo akiwa mtoto alikuwa akiimba kaswida katika madrasa pamoja na nyimbo nyengine huko shuleni. Habari hii imepatikana kutokana na mahojiano aliyoyafanya Nyongesa na Khadija mwaka (2013). Kwa sasa anaimba na kundi la TOT nchini Tanzania. Baadhi ya nyimbo za Khadija Kopa ni *Toroka Uje Night, Ngwinji, Mtie Muumeo Kamba, Mwanamke Mambo Utapenda, Unaringa Umepima, Nalijua Jiji, Topin Town, Mjini Chuo Kikuu, Lady with Confidence, Mambo Makubwa, Wigi Linawasha, Homa ya Jiji, Umeishiwa Full Stop, Kadandie Niliwaze, Nimemridhi, Mwanamke Jeuri, Nampenda Yeye Kiwembe. na Hutoweza Kuizima.*

Sababu iliyomsukuma mtafiti kufanya utafiti huu kwanza ni kwamba katika utalii alioufanya hakuona utafiti uliowahi kufanyika ukiwa na lengo la kuchunguza namna matumizi ya taswira yanavyotumika, miktadha ya utumiaji wa taswira hizo na athari zake kwa jamii katika nyimbo za taarab za mahaba za Khadija Kopa. Hivyo mtafiti aliona ipo nafasi ya kufanyika utafiti huu kwa lengo la kutaka kubaini namna nyimbo za taarab za mahaba za Khadija Kopa zinavyotumia matumizi ya taswira na namna miktadha mbambali inavyochochea kutumika kwa taswira hizo na athari zake kwa jamii.

## 1.3 Tatizo la Utafiti

Nyimbo ni utanzu wa kale na maarufu sana katika jamii yoyote ulimwenguni. Nyimbo zimekuwa zikifanya kazi ya kusawiri maisha halisi ya jamii ya Waswahili (Waziri, 2016). Watafiti wengi wamewahi kufanya uchunguzi kuhusu nyimbo za

jamii mbalimbali. Watafiti hao ni kama vile Khamis (1998), Amer (1998), Yego (2013), Moh`d (2015), Khamis (2016), Ali (2016), Njeri (2016), Waziri (2016), Khamis (2017), Otieno (2017), Abdalla (2018). Abdala (2018) alifanya utafiti wenye mada "Kuchunguza Dhamira na Fani katika Nyimbo za Taarab Asilia: Mifano ya Nyimbo za Shakila Said Khamis." Katika utafiti huo aligundua kwamba nyimbo hizo zimebeba dhamira kama vile mapenzi, ukombozi, utamaduni, usaliti, dini na imani, ukweli na uwazi, ukombozi, elimu na umalaya. Pia, kuna matumizi ya hali ya juu ya lugha. Utafiti wa Abdalla (2018) umemuongoza mtafiti kuchambua vipengele vya lugha katika nyimbo za taarabu za Khadija Kopa.Pia juhudi za watafiti hawa zimeibua ari ya kufanyika utafiti huu kutokana na ukweli kwamba pamoja na tafiti nyingi zilizowahi kufanyika katika utanzu wa nyimbo ilibainika kwamba hakukuwa na utafiti uliowahi kufanyika ukiwa na lengo la kuchunguza matumizi ya taswira katika nyimbo za mahaba za Khadija Kopa. Hivyo basi tatizo la utafiti huu lilikuwa ni kutaka kujua ni namna gani Khadija Kopa anatumia taswira na miktadha inayomsukuma mtunzi kutumia taswira hizo. Pia, mtafiti alitaka kujua jinsi matumizi hayo ya taswira yalivyo na athari kwa jamii. Kwa vile kipengele hicho hakijafanyiwa utafiti ni wazi kukamilika kwa utafiti huu kumeziba pengo hili la kitaaluma katika uwanja wa fasihi ya Kiswahili.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una lengo kuu na malengo mahususi kama ifuatavyo:

### 1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kubainisha taswira zilizopo katika nyimbo za Khadija Kopa na miktadha iliyopelekea kutumika kwa taswira hizo pamoja na athari zake kwa jamii.

### 1.4.2 Madhumuni Mahasusi

Utafiti huu una madhumuni mahasusi yafuatayo:

i. Kuaainisha taswira katika nyimbo za taarabu za Khadija Kopa.
ii. Kubainisha miktadha inayopelekea Khadija Kopa kutumia taswira hizo katika nyimbo zake.
**iii.** Kueleza athari za taswira za nyimbo za taarabu za Khadija Kopa kwa jamii.

## 1.5 Maswali ya Utafiti

i. Ni taswira zipi anazozitumia na Khadija Kopa katika nyimbo zake za taarabu?
ii. Ni miktadha ipi inayopelekea Khadija Kopa kutumia taswira hizo katika nyimbo zake?
iii. Je, taswira za nyimbo za taarab za Khadija Kopa zina athari gani kwa jamii?

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu una umuhimu kama ifuatavyo:

**Kitaaluma:** Matokeo ya utafiti huu yatafaa kuwa marejeleo kwa wasomi wa ngazi zote za taaluma ya fasihi. Wataalamu ambao ni walimu, wahadhiri katika taaluma ya fasihi, wataweza kutumia utafiti huu katika kuandika vitabu na makala ambazo zinahusu taarabu za mahaba hasa zile zinazomhusu msanii maarufu Khadija Kopa.

**Kijamii:** Utafiti huu utakuwa na umuhimu kwa wanajamii kwani utafiti huu utakuwa ni kumbukumbu ambapo nyimbo za Khadija Kopa zilizotafitiwa zitabakia katika maandishi na hivyo kutumika kwa kizazi cha sasa na baadae. Kama inavyotambulika kuwa fasihi simulizi imekuwa ikipotea ama kubadilika kutokana na mabadiliko

yanayoikumba jamii, hivyo utafiti huu ni sehemu ya urithi na kumbukumbu ya baadae.

## 1.7 Mipaka ya Utafiti

Waimbaji wa taarab katika jamii ya Waswahili ni wengi kama vile Shakila Khamis Said, Mzee Yussuf, Wazera, Khadija Omar Kopa, Omar Kopa, Isha Mashauzi na kadhalika. Kila mmoja kati ya wasanii hawa, amekuwa na nyimbo nyingi za taarab. Kwa mantiki hiyo kutafiti nyimbo hizo kwa wakati mmoja inakuwa vigumu. Kwa hivyo, mtafiti amechagua nyimbo za Khadija Kopa kutokana na kwamba yeye ni muimbaji anayeimba nyimbo za mahaba zaidi ukilinganisha na waimbaji wengine wa taarabu. Aidha, kwa vile muimbaji huyu ana jumla ya nyimbo 21 ambazo zimekuwa zikiimbwa na kusikilizwa katika jamii, mtafiti ameteua nyimbo tano ambazo ni *Niliwaze*, *Nimmeridhi*, *Mwanamke Mambo*, *I Love You* na *Full Stop*. Kutokana na ukweli kwamba baada ya kutumia mbinu ya usomaji makini mtafiti amebaini nyimbo hizi zinazo taswira ambazo zilimsaidia kujibu maswali ya utafiti huu hivyo kufikia malengo ya utafiti yakiwemo kuangalia taswira, miktadha ya matumizi ya taswira hizo pamoja na athari yake katika jamii. Katika kukamilisha malengo hayo, mtafiti aliongozwa na nadharia ya Simiotiki.

## 1.8 Changamoto za Utafiti na Utatuzi wa Changamoto

Mtafiti alikabiliwa na changamoto ya kusafiri kutoka eneo moja na jengine kutokana na kwamba mtafiti ni muajiriwa wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Pia, kwa kipindi hiki cha mlipuko wa homa ya mapafu inayosababishwa na virusi vya UVIKO-19 imekuwa ni vigumu kusafiri kutoka eneo moja hadi jengine. Hata hivyo, mtafiti amevitatua vikwazo hivi kwa kuomba ruhusa kwa muajiri wake kadri vile

inavyohitajika. Aidha, mtafiti amefuata maelekezo ya wataalamu wa afya kama inavyoelekezwa na serikali ili kufanikisha utafiti huu pale alipohitajika kusafiri kutoka eneo moja na jengine.

### 1.9 Mpangilio wa Tasnifu

Tasnifu hii ina sura tano. Sura ya kwanza inaeleza vipengele vya utangulizi ambavyo ni usuli wa mada ya utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, changamoto na utatuzi wa changamoto hizo na mpangilio wa tasnifu. Sura ya pili inaeleza mapitio ya kazi tanguzli na nadharia iliyomuongoza mtafiti kukamilisha utafiti huu. Sura ya tatu imebainisha mbinu za utafiti ambapo katika sura hiyo kuna vipengele kama vile eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, sampuli na usampulishaji, data na mbinu za kukusanya data, mbinu ya uchambuzi wa data, usahihi wa data, kuaminika kwa data na maadili ya utafiti. Sura ya nne inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti huu na sura ya tano ni muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu.

# SURAYA PILI

# UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MIKABALA YA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Mapitio ya kazi tangulizi ni utalii wa kina wa machapisho yanayohusu mada inayotafitiwa. Utalii huo hufanywa na mtafiti kwa nia ya kupata uelewa juu ya mada anayoitafiti. Pia, kuona pengo la utafiti linalohitaji kuzibwa. Hivyo basi, katika sehemu hii mtafiti amebainisha maandshi ya watafiti kama vile; Muhando na Balsidya (1976), Simiyu (2011), Yego (2013), Moh`d (2015), Mulokozi (1996), Mungai (2014), Hamad (2016), Khamis (2016), Mzee (2016), Njeri (2016), Waziri (2016), Rashid (2016), Gitonga (2017), Abdalla (2018), na Mohamed (2018) ambao wamewahi kufanya tafiti zao kuhusiana na nyimbo wakiwa  na malengo tofauti.

## 2.2 Ufafanuzi wa Dhana

Katika sehemu hii inafafanua dhana mbalimbali kama vile dhana ya nyimbo, dhana ya mahaba, dhana ya taswira, tafiti kuhusu nyimbo za taarabu, pengo la utafiti, na mkabala wa kinadharia.

### 2.2.1 Maana ya Nyimbo

Dhana ya nyimbo imekuwa na fasili nyingi miongoni mwa wataalamu. Mathalani, Mulokozi (1996) anasema kwamba wimbo ni kila kinachoimbwa. Maana hii huweza kuingiza hata tanzu ambazo ni za kinathari kama vile hadithi kuwa na sifa ya wimbo iwapo utaimbwa. Maana hii inakinzana na ile inayotolewa na baadhi ya wachambuzi wa kazi za fasihi ambao wanaona kuwa wimbo lazima utokane na utanzu wa ushairi kwani hicho ni kipera cha ushairi. Wenye kushikilia msimamo huu ni pamoja na Hamad na wenzake (1972) ambao wanaona kuwa nyimbo ni mashairi mafupi

yanayotambwa na wanajamii ambapo kimuundo huweza kuwa na ubeti mmoja au zaidi. Pia, kipera hiki huweza kuambatana na ala za muziki au bila kuwa na ala za muziki.

Vile vile, Msokile (1981) anafasili nyimbo kwa kusema kuwa ni mawazo yanayoimbwa na watu baada ya kusukumwa na nguvu maalumu. Wasanii huimba nyimbo baada ya kupata mguso fulani ndani ya jamii. Sanaa ya nyimbo inatafautiana na sanaa ya mazungumzo kwa sababu ya matumizi ya lugha pamoja na vionjo maalumu vya kishairi vinavyoleta mvuto kwa jamii. Mawazo haya yanafanana na yale ya Balisidya (1987) anayeeleza kuwa nyimbo ni tungo za kishairi, zenye kutumia mahadhi ya melodi, mapigo na muwala. Nyimbo huimbwa na watu ambao huwa na lengo la kuelezea maisha ya jamii husika.

Naye Simiyu (2011) anaeleza kuwa nyimbo ni tungo zenye mapigo au mawimbi na huweza kuimbika. Nyimbo husheheni mawazo mazito na hudhamiria kuonesha uhusiano wa kijamii, migogoro ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Kupitia nyimbo jamii hubadilika, huburudika, hujifunza, huongolewa, huomboleza na hupitisha amali zake na historia. Aidha, nyimbo huwa na uteule wake wa majukummu kwani hupitisha, hueleza na huathiria hisia za ndani za watu. Anaendelea kueleza kuwa nyimbo zina historia kongwe sana kwa watu kwani inakisiwa kuwa punde tu mwanadamu alipoanza kutumia lugha alianza kuimba mashairi. Mawazo haya yanayohusu ukale wa nyimbo yanaungwa mkono na wahakiki wengi wa kazi za fasihi. Mathalani, Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kwamba nyimbo zinatokana na ushairi ambao ndio utanzu wa fasihi ulio mkongwe, nyimbo zilianza na hisia za matukio yaliyowakuta watu katika mazingira yao ya raha na furaha, ugumu wa

kujituma ama machungu na ushujaa. Wanafafanua kwa kusema kuwa, katika jamii za kilimwengu wimbo ulianza wakati mwanadamu alipobuni lugha, jambo ambalo lilimtoa katika hali ya uhayawani na kumfanya awe kiumbe razini. Mabadiliko haya yalimfanya mwanadamu ayaelewe mazingira yake na aweze kutoa mchango katika kuyakabili na kuyabadilisha mazingira hayo.

Maelezo haya yanatupatia uelewa kwamba nyimbo ni utanzu wa fasihi simulizi ambao huwa na muundo wa kishairi lakini ushairi huo unaweza kuwa na urari wa vina na mizani ama usio na urari wa vina na mizani. Sifa moja ya nyimbo ni kuimbika, hivyo wimbo lazima uwe unaimbwa. Kuhusu historia mtafiti amejifunza kuwa huu ni utanzu wa kale kabisa katika maisha ya binadamu kwani ulianza mara tu baada ya mtu kujifunza lugha. Jambo linalohitaji mjadala zaidi hapa ni kwamba kwa sababu fasihi ni zao la jamii, hata nyimbo za mahaba zimekuwa na athari fulani kwa jamii.

### 2.2.2 Nyimbo za Mahaba

Nyimbo za mahaba ni nyimbo ambazo zimejikita kujadili mapenzi. Simiyu (2011) anaeleza kwamba mapenzi ni kitu kizuri sana na hivyo kuelezwa huhitaji lugha jamali. Nyimbo za mahaba ni nyimbo ambazo huhusu mapenzi. Nyimbo hizi hutumiwa najamii kupitisha hisia za moyoni na upeo wa mapenzi yao kwa wapendwa wao. Ingawa huimbwa na fanani mahususi, zinasimamia maoni ya jamii nzima kuhusu mapenzi. Anaendelea kueleza kwamba hisia hizo huweza kuwa za kufurahisha au kukasirisha pale fanani anapolenga kumsifu ama kumkashifu mpenzi wake. Baadhi ya nyimbo hizi hutungwa kwa namna ya usemezano kati ya mwimbaji na mlengwa anayewakilishwa na msaidizi wa mwimbaji. Nyimbo za mahaba pia zina

sifa ya kuonesha uozo wa jamii kama vile, wivu wa wanaowazunguka wale wanaopendana, hila za wapenzi wasiokuwa na mapenzi ya dhati, wapenzi wanaovunja ahadi zao, hivyo hutumiwa nyimbo hizi ili kuwakashifu.

Vile vile, Yego (2013) alipokuwa akifanya utafiti wenye mada "Nafasi ya Mwanamke: Jinsi Inavyotetewa katika Nyimbo za Taarab Zanzibar." anaeleza kwamba nyimbo ya *Tupendane Wabaya Waulizane* imekusanya tamaduni za wazawa kama vile; utamaduni wa chakula, mimea, ndege na michezo pamoja na dhamira za cheo, biashara na utabaka. Pia, katika nyimbo ya *Kibiriti Upele* amegundua dhamira ya nafasi ya mwanamke katika ndoa, dhuluma za mwanamke katika ndoa, uasharati, usaliti, talaka, uadilifu, werevu na umakinifu.

Maelezo haya yamempatia uelewa mtafiti kwamba nyimbo za mahaba huweza kuwa na athari ya ziada badala ya kusawiri mapenzi tu. Pamoja na watunzi wa nyimbo za mahaba kujikita zaidi kusawiri mapenzi lakini nyimbo zao huweza kuibua masuala mingine yanayoihusu jamii kama vile siasa, uchumi, imani na utamaduni. Hivyo kwa kutumia mawazo haya mtafiti ameweza kubainisha athari chanya na hasi zinazojitokeza katika nyimbo za taarab za kimahaba za Khadija Kopa.

### 2.2.3 Dhana ya Taswira

Taswira ni matumizi ya lugha ambayo hujenga picha katika ubongo wa msomaji ama msikilizaji. Mdungi (2000) anaeleza kuhusu dhana ya taswira kuwa ni lugha ambayo msomaji au msikilizaji humfanya aone, asikie, aonje, anuse au aguse kutokana na mawazo aliyoyasoma au kuyasikia. Anaendelea kueleza kwamba taswira huweza kuekwa katika matapo makuu matano ambayo nitaswira za kuona, taswira za kusikia,

taswira za kugusa, taswira za kunusa na taswira za kuonja. Hivyo kwa maana hii ya mdungi tunabaini kuwa taswira zinaangukia katika viungo vya hisia.

Naye Madumulla (2009) anaeleza kuwa taswira ni lugha inayochora picha ya vitu au mahali kwa kutumia ishara. Pia, anaendelea kusema kwamba taswira hupewa maana nyengine ili kuashiria kitu chengine. Ndio maana husemwa kwamba taswira ni uwakilishi. Kupitia maana hii mtafiti anaona kuwa Madumulla anaitazama taswira kama kipengele cha lugha ambacho huficha maana ya lugha iliyokusudiwa kwa kutumia ishara na kiashiriwa. Hivyo mawazo haya yalitumiwa na mtafiti ili kubainisha maana za taswira na namna zinavyoakisi jamii.

### 2.2.4 Mgawanyo wa Taswira

Kimsingi wachambuzi wametofautiana katika kuzigawa taswira kama zinavyotumika katika kazi za fasihi. Kezilahabi (1976) katika kazi yake ya "Ushairi wa Shaaban Robert" akinukuliwa na Senkoro (1988) katika Taufiq (2016) anaziweka taswira katika matapo makuu matatu. Tapo la kwanza huwakilishwa na taswira za maumbile. Hizi ni zile zenye kuonesha hali mbalimbali kama vile hali ya hewa ya angani, juu na chini ya ardhi. Tapo la pili ni lile la taswira zinazowakilishwa na viumbe hai kama vile binadamu, wanyama na wadudu. Tapo la tatu ni linahusisha taswira za viumbe dhahania kama vile majini na mashetani.

Naye Senkoro (1988) anaona kuwa taswira ni maneno yaliyopangwa na kuweza kuchora picha kamili ya kitu, hali, wazo, dhana au uzoefu fulani kwa jamii. Katika ufafanuzi wake anabainisha aina kuu tatu za taswira, ambazo ni taswira zinazoonekana, taswira za mawazoni na taswira za hisi. Ubainishaji huu unatumia vigezo tofauti na vile alivyovitumia Kezilahabi (1976) ambavyo vimeelezwa hapo

juu. Senkoro ametumia kigezo cha viungo vya hisia kama msingi wa kuzibainisha aina za taswira. Hivyo ufafanuzi wa aina hizo za taswira kwa kigezo cha hisia ni kama zifuatazo:

**Taswira Zionekanazo**

Hii ni aina ya taswira ambayo hujenga picha ya kitu katika ubongo wa msomaji ama msikilizaji. Maelezo yanayotolewa hujenga picha katika ubongo na hatimae msikilizaji au msomaji hupata maana kupitia taswira hizo.

**Taswira za Mawazoni**

Hii ni aina za taswira ambayo mtu huwaza akilini mwake. Mara nyingi hupatikana kutokana na matumizi ya lugha ya mafumbo yaliyotumika katika kazi ya fasihi. Matumizi ya taswira ya mawazoni huifanya hadhira itofautiane katika kuipa maana kazi ya fasihi. Hii inatokana na ukweli kwamba watu hutofautiana katika kuyafumbua mafumbo yanayohusu matumiz ya lugha ya fasihi.

**Taswira za hisi**

Hii ni aina ya taswira ambazo zinamfanya mtu ahisi mguso fulani unahusu jambo linalozungumziwa. Senkoro (1988) anaeleza kuwa taswira hizi hushughulikia hisi za ndani ambazo zinaweza kumfanya msomaji au msikilizaji aogope, akasirike, apate wasiwasi au kuhisi kichefuchefu.

Ubainishaji wa taswira unaofanywa na Senkoro kama ulivyoelezwa katika sehemu unaonesha kuwa umegusia maeneo muhimu matatu ya hisia, hata hivyo ubainishaji huo unaonekana kuwa na upungufu kutokana na kutoweka tapo linalohusisha taswira za muonjo na taswira za kusikia. Hivyo, mtafiti anaona kuwa ubainishaji huu

ungeweza kukamilika iwapo ungejumuisha taswira za kusikia na kuonja kama ilivyofanywa na Mdungi 2000. Kwa mantiki hiyo, utafiti huu kwa kutumia kigezo cha hisia unaona kuwa kuna taswira zinazoonekana, taswira za mawazoni, taswira za hisi, taswira za kusikia na taswira za mwonjo.

Mtaaalamu mwengine aliyewahi kuzibainisha taswira ni Wamitila (2003) ambapo anaeleza kuwa taswira zinaweza kuekwa katika makundi manne. Makundi hayo ni taswira kuu, taswira za kimaelezo, taswira ya kimsingi na taswira za kiishara. Ufafanuzi wa aina hizi za taswira ni kama ifuatavyo: Aina ya kwanza huwakilishwa na taswira kuu. Hii ni aina ya taswira ambayo hutumika kifasihi na huchukua nafasi kubwa katika kazi ya fasihi. Pia, taswira hizi huwa na uhusiano wa karibu na maudhui ya kazi inayohusika. Kwa maana nyingine huibua maudhui ya kazi husika.

Aina ya pili ni taswira za kimaelezo. Hii ni aina ya taswira ambayo hujengwa kutokana na maelezo ya mwandishi au lugha iliyotumiwa na mwandishi. Hii, humaanisha kuwa mwandishi hutumia lugha ambayo ina uwezo wa kujenga picha fulani katika akili ya msomaji au msikilizaji wake.

Aina ya tatu ya taswira ni taswira ya kimsingi. Hii ni aina ya taswira ambayo hutumika katika muundo wa kazi ya fasihi. Taswira hii nayo huathiri na kuitawala kazi husika. Kwa mfano, riwaya ya Nagona ya Kezilahabi imetumia aina hii ya taswira katika kuisuka kazi yake. Kwa mfano taswira kama vile ya paa, roho na mto zilivyochorwa kama taswira za kimsingi kwa kuweza kusawiri mambo mbalimbali katika jamii.

Aina ya nne ya taswira ni taswira ya kiishara. Hizi ni taswira ambazo hujengwa akilini mwa msomaji au msikilizaji wa kazi husika kutokana na namna msanii anavyotumia au kuteua maneno katika lugha. Pia, lugha anayotumia mwandishi kwa kawaida huwa na ujumbe wa ziada pamoja na kuashiriakitufulani. Aina hii ya taswira huonekana kufanya kazi kama ishara kutokana na kuwasilishwa kwake.

Kwa ujumla baada ya kutafakari kwa kina mtafiti ameona kuwa ubainishaji wa taswira unaofanywa na Wamitila kama ulivyoelezwa katika sehemu hii bado una utata mkubwa. Hii ni kwa sababu aina moja ya taswira huweza kujitokeza katika aina nyengine hivyo kuleta mkanganyiko. Kwa mfano tunapoangalia taswira kuu na taswira ya kiishara mpaka kati ya taswira hizi hauko bayana.

Kwa upande mwengine Khatib (2011) anao mtazamo tofauti juu ya aina za taswira. Yeye kwa upande wake anazibainisha taswira katika makundi sita. Makundi hayo yameelezwa na Taufiq (2016) ambayo kwanza, kuna taswira za kizuolojia ambazo ni taswira zinazohusiana na viumbe hai kama vile ndege, wadudu na wanyama. Aina mbalimbali za ndege, wanyama na wadudu huchorwa ili kuwakilisha tabia fulani ambazo zinaweza kuwa mbaya au nzuri. Mathalani, bundi huchorwa kuonesha nuksi au uchuro. Kasuku naye huonesha hali ya uropokaji au apendaye kuiga, wakati njiwa manga huonesha uzuri wa sura na uhodari wa kufanya mapenzi. Pia, taswira za wanyama ambazo zimeonesha wanyama wakiashiria matendo mazuri na mabaya. Pili, ni taswira za botania. Hizi ni aina za taswira zinazohusiana na mimea mbalimbali iliyopo katika jamii. Aidha, mimea nayo hutumika kuwakilisha masuala mbalimbali hasa kwa kutumia maua na matunda yake.

Tatu, ni taswira za kiastronomia. Aina hii ya taswira hubainisha vitu vitoavyo mwanga na kumeremeta kama vile jua, mwezi, nyota na sayari ambavyo vinaonekana katika anga la juu la dunia na huwezi kuvishika.

Nne, ni taswira za kijiolojia. Jiolojia ni taaluma ya kisayansi kuhusu gamba la ardhi, miamba, vito na madini. Vitu vya shaba, bati, chuma, dhahabu, almasi na vito. Tano, ni taswira za kiteolojia. Hizi ni taswira za kidhahania za kiimani ambazo hazionekani wala kushikika. Miongoni mwa vitu au viumbe hivyo ni kama vile Mungu, malaika, pepo na majini.

Sita, ni taswira za vitu vya kawaida. Hizi ni aina za taswira ambazo hutengenezwa na binadamu kwa uwezo wake binafsi kama vile kiti, kitanda, meza, jahazi na vingine vinavyofanana na hivyo ambavyo hutumika katika shughuli mbalimbali.

Baada ya kusoma kwa makini maandiko ya wataalamu hawa yanayohusu uainishaji wa taswira mtafiti ameona kuwa ubainishaji wa Khatib (2011) una ubora ukilinganishwa na ule wa wataalamu wengine kutokana na kwamba kila taswira inabainishika kwa uwazi zaidi katika tapo jengine jambo ambalo limepunguza utata katika ubainishaji huo. Hivyo katika utafiti huu mawazo ya Khatib ndiyo yaliyotumika katika kuzibainisha taswira zilizotumika katika nyimbo za mahaba za Khadija Kopa.

## 2.5 Tafiti Kuhusu Nyimbo za Taarab

Simiyu (2011) alifanya uchambuzi wa nyimbo za taarab. Baadhi ya nyimbo alizozifanyia uchambuzi ni kama vile *Najiamini Napendwa, Asumini* na *Chochote Kizuri Hakikosi Kasoro*. Katika uchunguzi wake amebaini kwamba sifa kuu ya

taarab ni matumizi ya mafumbo. Anazidi kufafanua kuwa nyimbo za taarab aghalabu hugusia suala la mapenzi. Katika uchambuzi wake ameziweka nyimbo hizo chini ya anuani ya *Nyimbo za Mahaba*. Aidha, katika uchambuzi huo alifanya uchambuzi wa kipengele cha dhamira. Uchambuzi huu utakuwa na faida katika kufikia lengo la utafiti huu kwa sababau umesaidia kuona ni jinsi gani vipengele vya lugha vinavyoweza kufanyiwa uchambuzi.

Yego (2013) alifanya utafiti kuhusu "Nafasi ya Mwanamke: Jinsi Inavyotetewa katika Nyimbo za Taarab Zanzibar." Lengo kuu la utafiti huo lilikuwa kuchunguza maudhui katika nyimbo za taarab za Kibiriti Upele na Tupendane Wabaya Waulizane. Vile vile, katika utafiti huo kulichunguzwa dhamira na vipengele vya fani kama vile tashbiha, kejeli, misemo na sitiari. Katika utafiti huo aligundua kwamba nyimbo ya *Tupendane Wabaya Waulizane* imekusanya tamaduni za wazawa kama vile; utamaduni wa chakula, mimea, ndege na michezo pamoja na dhamira za cheo biashara na utabaka. Katika nyimbo ya *Kibiritia Upele*. Yego amegundua dhamira ya nafasi ya mwanamke katika ndoa, dhuluma za mwanamke katika ndoa, uasharati, usaliti, talaka, uadilifu, werevu na umakinifu. Utafiti huu umekuwa na umuhimu mkubwa katika kufikia lengo la utafiti uliofanyika. Utafiti wa Yego umefanya uchambuzi wa vipengele vya lugha ambavyo vimefanyiwa uchambuzi namna vinavyotumika katika nyimbo. Hivyo mtafiti ameutumia utafiti huu kama kielelezo kilichomsaidia kufikia malengo ya utafiti huu.

Rajab (2016) alifanya utafiti wenye mada "Kuchunguza Chanjo za Mapenzi katika Nyimbo za Taarab za Seif Salim." Katika utafiti huo aligundua kwamba nyimbo hizo zimesheheni chanjo zinazoibua hisiya za mapenzi kama vile; mapenzi ya dhati,

mapenzi ya udanganyifu, mapenzi ya ndoa, mahaba nakadhalika. Pia, chanjo ambazo alizigundua ni chanjo za mguso, chanjo za hisia, chanjo za mnuso na chanjo za ishara. Utafiti huu ulimsaidia mtafiti katika kuona ni jinsi gani taswira zinavyoonesha au kuakisi yale yaliyomo katika jamii kwani ametumia taswira ya chanjo kuyazungumzia mapenzi na jinsi yanavyoleta athari katika jamii na ulimwengu wa wale wanaopendana.

Khamisi (2016) alifanya utafiti kuhusu mada isemayo; "Kuchunguza Dhamira za Nyimbo za Siti Bint Saad." Katika utafiti huo aligundua kuwa nyimbo za taarab za Siti Bint Saad zimesheheni dhamira za matabaka, utamaduni na mapenzi. Pia, utafiti huo ulibaini kuwa kuna utajiri mkubwa wa matumizi ya mbinu za kisanaa kama vile masimulizi, takiriri, tashbiha, sitiari, misemo na mwingiliano tanzu ndani ya tanzu.

Utafiti huu ingawa ulijikita kutafiti nyimbo za mwimbaji tofauti na yule aliyetafitiwa umemsaidia mtafiti kufikia lengo la utafiti anaotarajia kuufanya. Hii ni kutokana na ukweli kwamba utafiti huo ulijikita kuchunguza vipengele vya lugha taswira ikiwemo kama ilivyokuwa kwa utafiti huu. Kwa kufanya hivyo imekuwa rahisi kulifikia lengo la utafiti huu.

Njeri (2016) alifanya utafiti wenye mada "Mwingiliano Tanzu katika Modern Taarab-Mipasho." ya jamii ya Tanzania. Katika utafiti huo iligundulika kwamba kuna udhaifu wakuzibainisha nyimbo za taarab. Pia, ilibainika kuwa nyimbu hizo zina dhima ya kuhifadhi na kurithisha utamaduni, kuleta umoja miongoni mwa jamii na hutumika kuburudisha watu. Vile vile, taarabu za kisasa zimekuwa zikitumia vipengele vya fasihi simulizi ambavyo hulinganisha na kutofautisha mitindo tofauti ya taarab za kisasa. Utafiti wa Njeri pia umemsaidia mtafiti kufikia lengo la utafiti

huu. Kwanza, mtafiti amejifunza namna data zinazohusu athari za matumizi ya taswira kwa jamii. Pili, mtafiti ameona namna data zinazohusiana na vipengele vya fani zinavyojitokeza katika nyimbo za taarab.

Utafiti mwengine uliojikita kuchunguza nyimbo za taarab ni ule wa Otieno (2017), ambaye alifanya utafiti wenye mada "Uchanganuzi wa Kipragmatiki wa Sitiari katika Nyimbo za Taarab: Mifano kwa Mzee Yussuf na Mwanahawa Ally, Unguja." Utafiti huu ulikuwa na lengo kuu la kufumbua maana za sitiari katika mutrib wa taarab teule. Matokeo yalionesha kuwa watribu wa nyimbo za taarab huwasilisha ujumbe wao kisitiari. Vile vile, ilibainiska kwamba nyimbo hizi hutekeleza zaidi majuku kadhaa yakiwemo kumwirika mahusiano na changamoto ziliomo katika jamii. Zaidi ya hayo iligundulika kwamba maana kusudiwa katika nyimbo za taarabu inaweza kuelezewa kwa kutegemea misingi ya kiuamali. Pia, mawasiliano hutumia njia ya kusimba maana. Utafiti huu pia umetoa msingi imara wa kufikia lengo la utafiti na ni chanzo cha tatizo la utafiti huu kutokana na kuonesha kwamba nyimbo za taarab hazitumii lugha ya wazi. Ni kutokana na hilo ndio maana mtafiti ana lengo la kutathmini namna nyimbo za taarab zinavyotumia taswira katika miktadha mbalimbali na athari za taswira hizo kwa jamii.

Mtaalamu mwngine aliyewahi kuchunguza nyimbo ni Abdala (2018) ambaye alifanya utafiti wenye mada "Kuchunguza Dhamira na Fani katika Nyimbo za Taarab Asila: Mifano ya Nyimbo za Shakila Said Khamis." Katika utafiti huo aligundua kwamba nyimbo hizo zimebeba dhamira kama vile mapenzi, ukombozi, utamaduni, usaliti, dini na imani, ukweli na uwazi, ukombozi, elimu na umalaya. Pia, mtafiti aligundua kwamba nyimbo hizo zinatumia mbinu za kisanaa kama kejeli, tshtiti,

majazi, taswira na ishara na takiriri. Vile vile, nyimbo hizo zimesaniiwa kwa kufuata kanuni za kimapokeo.

Utafiti wa Abdala (2018) umemsaidia mtafiti kuona namna suala la miktadha na matumizi ya taswira na athari zake kwa jamii linavyoweza kujitokeza katika nyimbo za taarab na hatimae kufanyiwa uchambuzi. Pengo la utafiti huu na ule wa Abdala ni kwamba yeye alifanya uchunguzi wa nyimbo za Shakila lakini utafiti huu utajikita kuchunguza nyimbo za mahaba za Khadija Kopa katika kipengele kikuu cha taswira.

Mtafiti mwengine aliyefanya utafiti katika nyimbo za taarab ni Khamisi (2017) ambaye alikuwa na mada "Mabadiliko katika Nyimbo za Taarab na Uwasilishaji wake kulingana na Wakati." Katika utafiti huo aligundua kuwa vipindi mbalimbali vya kihistoria kama vile kipindi cha utawala wa Sultani, kipindi cha harakati za mapinduzi na uhuru, baada ya mapindiuzi hadi sasa ndivyo vilivyoathiri moja kwa moja nyimbo za taarab. Mathalani, wakati wa mapinduzi nyimbo hizo zilikuwa zikitungwa na kuimbwa papo kwa papo. Utafiti huu pia una umuhimu mkubwa kwa mtafiti kutokana na kuona namna nyimbo za taarab zinavyoweza kubadilika kutokana na miktadha ya kijamii. Hivyo mtafiti amechunguza namna taswira zilivyotumika na miktadha ya ubunifu wa taswira hizo ikiwa ni pamoja na atahari za taswira hizo kwa jamii.

## 2.6 Pengo la Utafiti

Mtafiti alitalii machapisho kadhaa yanayohusu mada iliyotafitiwa. Machapisho hayo yamejikita kufanya uchunguzi wa vipengele mbalimbali vya fani na maudhui katika nyimbo kama sehemu ya fasihi. Hata hivyo, mtafiti hakuona kazi iliyowahi kufanyika ikijikita kuchunguza matumizi ya taswira na miktadha inayopeleklea

kuibuka kwa matumizi ya taswira hizo na athari zake kwa jamii katika nyimbo za mahaba za Khadija Kopa. Hivyo basi mtafiti aliona ipo haja ya kufanyika utafiti huu ili kubaini namna Khadija Kopa anavyotumia taswira katika nyimbo zake za mahaba.

## 2.7 Mkabala Wa Kinadharia

Sengo (2009) anaifasili dhanna ya nadharia kuwa ni muongozo wa mawazo au maarifa yanayofasili taaluma mahsusi kwa kutoa maoni, mwelekeo au falsafa juu ya matumizi ya taratibu za utafiti. Hivyo katika utafiti huu, mtafiti ameongozwa na nadharia ya Simiotiki. Nadharia hii imefanyiwa uchambuzi na uwasilishaji kama ifuatavyo:

### 2.7.1 Nadharia ya Simiotiki

Wamitila (2002) anaeleza kuwa Simiotiki ni neno la lugha ya Kiyunani lenye maana ya ishara na ambalo linatumika kueleza mielekeo na makundi fulani ya kihakiki. Makundi hayo na mielekeo hiyo imezuka na mtindo wa kuzihakiki kazi za kifasihi ambapo unaangaza ishara katika kazi hizo. Kuzuka kwa nadharia hii kunahusishwa kwa kiasi kikubwa na miaka ya 1970. Wakati huo kulikuwa na mwelekeo mkubwa wa kuuasi na kuuwacha umuundo ambao ulikuwa umeutawala uhakiki wa kifasihi katika miaka ya 1960. Licha ya kuzuka kwake wakati wa simiotiki imefaidi kutokana na mawazo ya mwanaisimu wa Ki-swizi, aliyejulikana kwa jina la Ferdinand de Saussare ambaye inasemekana ndie mwanzilishi wa nadharia hii na aliungwa mkono na mwanafalsafa wa Kimarekani aliyejulikana kama Charles-Pierce ambaye nae anahusishwa na kielelezo cha ishara kinachohusishwa na pembe tatu ambazo ni ishara, yambwa  na kifasiri. Kwa mujibu wa mwanafalsafa huyu kila ishara huwa yambwa au kitendwa kinachorejelewa.

Kifasiri ni kile kinachochochewa katika akili ya anayeifasiri ishara hiyo. Kimsingi tunaweza kusema hii ni nadharia inayoshughulika na ishara na uashiriaji katika kazi za kifasihi. Mwelekeo mkubwa wa nadharia kupendelea neno matini unawafanya baadhi ya wahakiki kuiita nadharia ya umatini.

Sambamba na hilo, pia mwanafalsafa huyo amekuwa muhakiki muhimu katika kuweka misingi mikuu ya nadharia hii. Mawazo yake pamoja na Julia Kristeva yameacha athari kubwa katika uhakiki wa ishara na uashiriaji katika kazi za kifasihi. Dhana moja muhimu iliyohusishwa na Baithes ni msimbo. Kwa mujibu wa mawazo ya mtaalamu huyu, kila leksia hudhihirisha misimbo au kaida fulani ambazo huwa muhimu katika kuifasiri. Ifuatayo ni misimbo ya nadharia ya Simiotiki.

#### 2.7.1.1 Misimbo ya Nadharia ya Simiotiki

Barthes (1994) anaeleza kwamba kuna aina tano za misimbo inayotumika katika kazi za fasihi ambazo kwa pamoja huunda nadharia ya simiotiki. Aina hizo ni msimbo wa kimatukio, msimbo wa kihenemetiki, msimbo wa ki-seme, msimbo wa kiishara na msimbo wa kiurejelezi. Nadharia ya Simiotiki haiwezi kukamilika bila ya kurejelea mawazo ya Barthes kuhusu misimbo mitano ya usomaji ambayo ni miongoni mwa mihimili mikuu ya nadharia hii. Mtaalamu huyu anafafanua misimbo mitano kama ifuatavyo:

**Msimbo wa Kimatukio**: Huu unahusisha jinsi msomaji anavyouunda na kuuelewa msuko wa kazi hiyo kwa kuangalia jinsi matukio hayo yanavyofuatana kiathari au kisabasishi.

**Msimbo wa Kihemenetiki**: Huu nao unahusu taharuki na unajulikana na baadhi ya wahakiki kama msimbo wa kusimulia au kutamka hadithi. Msimbo huu unaweza kufumbatwa kwenye anuani ya kazi za kifasihi.

**Msimbo wa Ki-seme**: Msimbo huu unahusiana na jinsi msomaji atakavyoishia kuipata picha ya muhusika fulani wa kifasihi.

**Msimbo wa Kiishara**: Huu ni msimbo muhimu katika usomaji na uhakiki wa kazi za kifasihi. Msimbo huu unahusishwa na jinsi ambavyo wasomaji wanaovumbua maana ya kiishara katika kazi za kifasihi.

**Msimbo wa Kiurejelezi**: Msimbo huu unajengwa kutokana na viashiria vya utamaduni unaorejelewa katika kazi inayohusika. Urejeshi huu huunda uhalisi mahususi kutokana na matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji na kwa njia hiyo huipa kazi fulani nguzo kitamaduni.

Misimbo hii imetoa chachu kwa mtafiti kuchambua vipengele vya ishara na taswira kama zilivyojitokeza katika nyimbo za taarabu za Khadija Kopa.

Baadhi ya wahakiki kama vile Wamitila (2008) wamekuwa wakikosoa nadharia ya Simiotiki kutokana na nadharia hiyo kujikita zaidi kuchambua vipengele vya fani kuliko maudhui. Pamoja na kasoro hiyo mtafiti ataitumia misimbo ya Kiishara, msimbo wa Ki-seme na Kiurejelezi ambayo anaamini kwamba itafaa katika kufanya uchambuzi wa malengo ya utafiti huu. Msimbo wa Kiishara utatumika katika lengo la kwanza la utafiti huu ambalo linahusu ubainishaji wa ishara na taswira katika nyimbo za Khadija Kopa. Aidha, msimbo wa Kiurejelezi na Msimbo wa Ki-seme

itatumiwa na mtafiti katika uchambuzi wa lengo la pili na latatu ambayo yanahusu miktadha iliyopelekea kutumika kwa taswira hizo pamoja na athari zake kwa jamii. .

## 2.8 Hitimisho

Sehemu hii inaeleza mambo muhimu yanayojitokeza katika imefa  mapitio ya kazi tangulizi na nadharia iliyomuongoza mtafiti kufanya utafiti huu hadi kukamilika. Mtafiti ametalii machapisho mbalimbali ambayo yamemuwezesha kubainisha pengo la utafiti huu ambalo linatoa uthabiti wakuwepo mwanya wa kufanya utafiti huu.

# SEHEMU YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sehemu hii imefanya ufafanuzi wa vipengele vinavyohusu mbinu za utafiti zilizotumiwa na mtafiti. Kwa hivyo sehemu hii imewasilisha eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, mbinu za ukusanyaji data, uthabiti na kuaminika kwa data, mbinu za uchambuzi wa data na hitimisho.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu umefanyika katika nyimbo za taarabu za mahaba za Khadija Kopa. Eneo hili limechaguliwa na mtafiti kutokana na ukweli kwamba Khadija Kopa ni mtunzi na mwimbaji manju katika tathnia ya nyimbo za taarab za mahaba. Hata hivyo, mtafiti baada ya kusoma kwa kina mapitio ya kazi mbalimbali amebaini kuwa nyimbo za msanii huyu bado zilikuwa hazijafanyiwa uchunguzi katika kipengele cha taswira na miktadha inayomsukuma mwimbaji huyo kubuni taswira pamoja na athari ya taswira hizo kwa jamii. Hivyo mtafiti aliona ipo haja ya kufanyiwa utafiti eneo hilo.

## 3.3 Usanifu wa Utafiti

Utafiti huu umetumia muundo wa kimaelezo. Utafiti unaotumia muundo wa kimaelezo huwa data za utafiti huo zimekusanywa, kuwasilishwa na kufanyiwa uchambuzi kwa njia ya maelezo. Katika kuifafanua dhana hii Enon (1999) anaeleza kuwa utafiti huwa na muundo wa kimaelezo iwapo data zitawasilishwa kwa kutumia maelezo bila ya kutumia tarakimu. Hivyo mtafiti amechagua mbinu hii kwa vile huu ni utafiti wa kifasihi ambao hujikita zaidi katika sanaa ya maneno.

### 3.4 Walengwa wa Utafiti

Walengwa wa utafiti ni kundi lote ambalo linatarajiwa kutafitiwa. Kwa mujibu wa Enon (1998) anasema walengwa wa utafiti ni jumla ya watu, wanyama au vitu ambavyo vimekusudiwa kufanyiwa utafiti. Katika utafiti huu walengwa wa utafiti ni nyimbo za taarab za mahaba za Khadija Kopa. Mtafiti ameamua kufanya utafiti huu kutokana na ukweli kwamba msanii teule ni maarufu sana katika tathnia ya nyimbo za taarab na gwiji wa nyimbo za taarab za mahaba kama anavyoelezwa na Adungo (2019) kwamba msanii huyu ni bingwa wa kusisitiza umuhimu wa maadili katika masuala ya unyumba kwa matumizi ya Kiswahili fasaha na wingi wa busara mambo haya huyaeleza kwa kutumia methali, taswira, mafumbo na misemo katika uimbaji na utunzi wa nyimbo za taarab. Sifa hizi zimemfanya awe ni mwimbaji mwenye upekee anapolinganishwa na waimbaji wengine wa taarab. Pamoja na umuhimu wa msanii huyu kipengele cha matumizi ya taswira namiktadha inayopelekea ubunifu wa taswira hizo na athari zake kwa jamii ilionekana bado haijatafitiwa. Kwa mantiki hiyo, mtafiti aliona ipo nafasi ya kufanya utafiti huu.

### 3.5 Sampuli na Usampulishaji

Katika Utafiti huu Sampuli na Usampulishaji inafafanuliwa kuwa ni:

#### 3.5.1 Sampuli

Sampuli ni kundi dogo linalotarajiwa kutoa data zitazojibu maswali ya utafiti husika. Katika utalii uliofanywa na mtafiti imebainika kwamba Khadija Kopa ana nyimbo 21. Katika hizo 21 mtafiti ameona nyimbo 12 ambazo zimejikita katika mahaba. Hivyo mtafiti amechagua nyimbo tano kati ya hizo kama ni Sampuli ya utafiti huu. Nyimbo hizo ni *Nimemridhi*, *Niliwaze*, *Mwanamke Mambo*, *I Love You* na *Full Stop*.

### 3.5.2 Usampulishaji

Usampulishaji nikitendo cha kuwateua watu au vitu ambavyo vitampatia data mtafiti. Enon (1998) anaeleza dhana hii kuwa nimchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka kundi kubwa ambalo litafanyiwa uchunguzi. Upatikanaji wakundi hilo hutumia mbinu ya uteuzi wa nasibu au usio nasibu. Kothari (2004) anasema kwamba usampulishaji nasibu hutoa fursa kwa kila mtafitiwa kuwa na fursa sawa ya kuweza kuteuliwa kushiriki katika kutoa data zinazohitajika. Kwa upande mwengine usampulishaji usiokuwa nasibu hautoi fursa sawa kwa watafitiwa ya kupata nafasi ya kutoa data. Hii ni kwa sababu kunakuwa na sifa maalumu zinazohitajika awe nazo mtafitiwa. Zipo mbinu kadhaa ambazo hutumiwa katika uteuzi wa sampuli, lakini utafiti huu umetumia mbinu ya uteuzi wa sampuli kwa malengo maalumu.

#### 3.5.2.1 Mbinu ya Uteuzi wa Madhumuni Maalumu

Uteuzi wa madhumuni maalumu hutumiwa na mtafiti akiwa na lengo la kuteua sampuli kutokana na kuamini kwamba kundi analoliteua litampatia data anazozikusudia. Enon (1998) anasema kwamba mbinu ya uteuzi wenye malengo maalumu ni aina ya uteuzi wa data ambapo mtafiti huchagua watafitiwa wa kumpatia data kutegemea vigezo maalumu. Uteuzi huu unafaida ya kupunguza muda wa kutafuta watafitiwa. katika utafiti huu Mtafiti ametumia mbinu hii kwa sababu kwa kupitia visahani vilivyohifadhi nyimbo za taarabu za msanii Khadija Kopa na mtanadao wa “You Tube” msanii ameweza kuzisikiliza nyimbo sa msanii huyu na kuchagua zile tu ambazo zimempatia data kulingana na malengo mahususi ya utafiti. Nyimbo hizo ni *Nimmeridhi, Niliwaze, Mwanamke Mambo, I Love You* na *Full Stop.*

## 3.6 Data za Utafiti

Katika utafiti wowote wa kisayansi mtafiti hukusanya data za msingi na data za upili. Katika utafiti huu mtafiti amekusanya data za msingi na za upili ili kukamilisha malengo ya utafiti huu. Hivyo katika sehemu inayofuata mtafiti ameeleza namna data za utafiti huu zilivyokusanywa.

### 3.6.1 Data za Msingi

Data za msingi ni data ambazo zinakusanywa kwa mara ya kwanza na mtafiti na hazijatumika na mtafiti mwengine kwa lengo la utafiti kama unaofanyika. Furlong (2000) anaeleza kwamba data za msingi ni zile zinazokusanywa kwa mara ya kwanza na mtafiti. Kwa kawaida data hizo huwa hazijakusanywa kama sehemu ya utafiti mwengine wowote. Young (1984) anafafanua dhana ya data za msingi kwa kueleza kuwa ni aina ya data ambazo huwa zinatarajiwa kujibu maswali ya utafiti unaotarajiwa kufanyika. Data hizo zinapofanyiwa uchambuzi na kuandikwa kama sehemu ya tasnifu hugeuka na kuwa data za upili. Katika utafiti huu, data za msingi zimekusanywa na mtafiti kutoka katika kanda za kunasia sauti na mtanado wa “You Tube” ambazo zimetumika kuhifadhi nyimbo za Khadija Kopa.

### 3.6.2 Data za Upili

Data za upili ni zile ambazo tayari zilikwishakusanywa na watafiti wengine kwa ajili ya kutimiza malengo ya utafiti wao na kuandikwa katika ripoti, makala, majarida, wavuti na vitabu, tayari kwa ajili ya kusomwa kama marejeleo katika maktaba mbali mbali (Creswell, 2009). Enon (1998) anaeleza kuwa data za upili hutumiwa na mtafiti katika kuandika pendekezo la utafiti na ndizo humpatia mtafiti pengo la utafiti wake. Vile vile, data za upili hutumika katika kushadidia data za msingi

wakati wa kuandika sura ambayo inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data zautafiti. Hivyo data za upili za utafiti huu zimepatikana kutoka katika majarida, tasnifu, wavuti na tovuti pamoja na vitabu ambavyo vimezungumzia mada ya utafiti huu.

### 3.7 Mbinu za Kukusanya Data

Mbinu za kukusanya data ni njia atazozitumia mtafiti kuzikusanya data za utafiti. Kothari (2004) anaeleza kuwa mbinu ya ukusanyaji data ni zoezi la awali katika utafiti ambalo humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kufanikisha lengo lake la utafiti. Katika utafiti huu mtafiti ametumia mbinu moja tu ya upitiaji wa nyaraka katika kukusanya data za utafiti huu. Namna mbinu hii ya upitiaji wa nyaraka ilivyotumika imeelezwa kama ifuatavyo:

#### 3.7.1 Mbinu ya Upitiaji wa Nyaraka andishi

Neno “nyaraka” kama lilivyotumika katika utafiti huu ni machapisho, kumbukumbu za vinasa sauti, na maandiko yanayopatikana katika maktaba. Kothari (2004) anaeleza kwamba mbinu ya upitiaji wa nyaraka maktabani ni mbinu ya kukusanya data kwa mtafiti kupitia machapisho yanayohusiana na mada inayotafitiwa. Mbinu hii inaonekana ni rahisi kwa mtafiti ili kukusanya data za upili na data za msingi. Mtafiti amechagua mbinu hii kutokana na ukweli kwamba ni rahisi kukusanya data kutokana na kwamba nyimbo za Khadija Kopa zipo katika vinasa sauti na katika mtandao wa *You Tube*. Pia, kwa kupitia mbinu hii mtafiti ametalii machapisho kadhaa yaliyotoa uelewa wa awali kuhusu mada ya utafiti huu. Zana zilizotumika kukusanyia data ni simu kwa ajili ya kupakua na kukusanya data za nyimbo za

Khadija Kopa na shajara kwa ajili ya kunukuu nyimbo pamoja na kupanga data zinazohusu maswali ya utafiti huu.

## 3.8 Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data ni mchakato wa kuzipanga data zilizokusanywa kutegemea malengo ya utafiti. Kothari (2004) anaeleza kuwa ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo itasaidia kujibu maswali ya utafiti husika. Katika utafiti huu data zimekusanywa na mtafiti, kuwasilishwa na kuchambuliwa na hatimae kufanyiwa uchambuzi, ambapo mtafiti ametumia shajara alililoligawa katika sehemu kuu nne. Sehemu ya kwanza ya shajara hiyo imeandikwa nyimbo zilizokusanywa, sehemu ya pili imenukuliwa aina za taswira kutoka katika nyimbo zilizokusanywa, sehemu ya tatu imenukuu taswira na miktadha ya matumizi ya taswira hizo na sehemu ya nne inahusu athari ya taswira hizo kwa jamii.

## 3.9 Hitimisho

Sehemu hii inahusu mbinu za utafiti. Katika sehemu hii mtafiti amebainisha mbinu za utafiti alizotumika hadi utafiti kukamilika. Mjadala wa vipengele vya mbinu za utafiti vilivyobainishwa ni eneo la utafi, usanifu wa utafiti, sampuli na usampulishaji, data na mbinu za kukusanya data na hitimisho.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

## 4.0 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti amefanya uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti zilizokusanywa katika nyimbo teule. Sura hii imegawika katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza imebainisha aina ya taswira zinazotumika katika nyimbo za taarabu za mahaba za Khadija Kopa. Sehemu ya pili imebainisha miktadha inayomsukuma Khadija kopa kutumia taswira katika nyimbo zake za taarab za kimahaba. Na sehemu ya tatu inahusu athari za matumizi ya taswira hizo kwa jamii. Uchambuzi wa data umeongozwa na nadharia ya Simiotiki. Nyimbo zilizotumika kama ni sampuli ya utafiti huu ni *Niliwaze, Nimemridhi, Mwanamke Mambo, I Love You,* na *Full Stop*.

## 4.1 Taswira katika Nyimbo za Taarab za Khadija Kopa

Lengo mahususi la kwanza la utafiti huu lililenga kuwasilisha na kufanya uchambuzi wa taswira katika nyimbo za taarab za mahaba za Khadija Kopa. Lengo la kuziangalia taswira katika kazi hii ni kutaka kubaini ni taswira zipi zimetumika katika nyimbo hizo. Matumizi hayo ya taswira kwa ujumla wake yamewasilishwa na kufanyiwa uchambuzi kwa kueleza maana zake kwa kuongozwa na taswira za Khatib (2011) na Taufiq (2016) katika tafiti zao kama ifuatavyo:

## 4.2 Taswira za Kizuolojia

Hizi ni aina za taswira ambazo huhusu viumbe hai kama ndege, wadudu na wanyama. Data zilizokusanywa na mtafiti zilionesha kuwa nyimbo za taarabu za Khadija Kopa zina matumizi ya aina hii ya taswira. Taswira hizi zimebainishwa katika jadwali kama ifuatavyo:

**Jadwali Na. 4.1.1 Taswira za Kizuolojia Katika Nyimbo za Taarab za Khadija Kopa**

| Na ya Nyimbo | Jina la Nyimbo | Taswira | Maana |
|---|---|---|---|
| 2 | Nimemridhi | Mtoto | Mrembo |
| 3 | Mwanamke Mambo | Paka | Adui |
| | | Mwanamke | Mwanamke mwenye mvuto |
| | | Buzi | Mwanamme anayefanya ngono na kulipa pesa |
| | | Bibi | Mpenzi |
| | | Golira | Mtu mwenye kudharaulika |
| 4 | I Love You | *Baby* | Mpenzi |
| | | Mpenzi | Mwanamme wake |
| 5 | Full Stop | Sharobaro | Vijana wanaopenda maisha ya anasa |

**Chanzo: Data Kutoka Nyimbo za Taarab za Khadija Kopa, Aprili, 2020**

Katika nyimbo hizo kuna taswira ambazo zinajengwa kwa kutumia viumbe hai. Utokeaji wa taswira hizi zinajidhihirisha katika mifano ya aina kwa aina. Kwa mfano, katika wimbo wa *Nimemridhi* kuna taswira ya "mtoto." Taswira hiyo inajidhihirisha kama ifuatavyo:

> Mwalilia wivu nimepata kitu bomba mie
> Kazi kwenu wachovu sasa mambo yangu laivu mie
> **Mtoto** bado nalipa na ngoma za uhakika
> **Mtoto** naserebuka namwagia mahaba mie
> Nna mkuna nyayoni maraha mpaka kichwani
> Sasa mwalilia wivu nimepata kitu bomba mie
> Zingatia mafundisho bibi alonifundisha

Neno "mtoto" linatolewa ufafanuzi na BAKIZA (2010) kwamba ni mtu mwenye umri wa chini ya miaka kumi na nane (18). Katika wimbo huo, taswira ya "mtoto," imetumiwa na muimbaji kuonesha kwamba bado yuko katika rika la vijana na hivyo anaweza kuvutia mbele ya wanaume ndio maana anasema "Mtoto bado nalipa na

ngoma za uhakika." Mfano mwengine wa taswira ya kizuolojia imetumika katika wimbo wa Mwanamke Mambo. Katika wimbo huo kuna taswira inayojengwa kwa kutumia neno "bibi." Taswira hii inajidhihirisha kama hivi:

Ukiumwa kajinyonge weye
Nyumba utaniachia
Simtoi hata chembe
Chepeto mchepeto
Umemchagua
Hutokula hutokula **bibi** peke yako

Kamusi ya BAKIZA (2010) inalifasiri neno "bibi" kuwa ni mzazi wa kike wa mama au wa baba. Katika ubeti huo, "bibi" ni taswira yenye kusawiri mwanamke yoyote aliyemo katika uhusiano wa ndoa. Aidha, katika wimbo huo kuna matumizi ya taswira ya "paka" pale muimbaji ambapo matumizi haya ya taswira yanajitokeza kama ifuatavyo:

Chumbani ukimfungia
Nitamuinda kama **paka**
Dirishani nitamtoa
Sitishwi nikitishika
Raha zimenikolea
Sitishwi nikitishika
Raha zimenikolea
Paka changu paka dada
Auti nimekutoa

Katika dondoo hilo, "paka" ni taswira ya kizuolojia ambayo ina maana ya "kitu kinachokera." Ingawa Gibe (1982) anaeleza kuwa taswira ya paka katika jamii imekukuwa ikitumika ikisawiri dhana tofauti tofauti. Pamoja na ukweli huo, mtafiti amebaini kwamba muimbaji anaposema "Nitamuinda kama paka," anafananisha na mtu anapomtafuta paka ambaye tayari ameharibu kama vile kitoeo ndani ya nyumba.

Kwa kutumia taswira hii tunapata picha ya namna msanii anavyodhamiria kumtafuta mpenzi wake.

Matumizi ya mbinu ya taswira ya kizuolojia pia yametumika katika wimbo wa *Mwanamke Mambo* kutokana na matumizi ya neno "mwanamke" pale mwimbaji anaposema "**Mwanamke** Mambo." Katika taswira hii tunajengewa picha ya namna mwanamke anavyotakiwa kuwa amekamilika na kuwa na umbile linalovutia kutegemea itikadi ya wanajamii. Vile vile, katika wimbo wa *Mwanamke Mambo* kuna matumizi ya taswira ya "golira." Taswira hii inaelezwa kama inavyojidhihirisha katika ubeti ufuatao:

Jicho mwanangu halooo
Jicho mwanangu halooo
Sio wewe ulokuruka
Shepu ya **golira** chapwaa
Mie *Beautiful*
*Beautiful natural*
Sio mkorogo ulojipaka
Sio mkorogo ulojipaka

Katika dondoo hilo hapo juu kuna matumizi ya taswira ya kizuolojia kutokana na mtunzi kutumia neno "golira." Hawa ni aina ya nyani wanaopatikana katika visiwa vya Zanzibar ambao ni miongoni mwa jamii ya kima. Hivyo basi, mwimbaji anaposema "Shepu ya golira chapwa" analengo la kukejeli na kudhihaki umbo la mwanamke mwengine kwa kulifananisha na golira.

Vile vile, katika wimbo wa *Mwanamke Mambo* kuna matumizi ya taswira ya kizuolojia kutokana na matumizi ya neno "buzi." Neno hili hutumiwa kama msimu wa lugha ya Kiswahili ambalo lina maana ya mwanamme anayefanya mapenzi ya nje ya ndoa. Hivyo taswira hii inaelezwa hivi:

Lipi anataka msaada na bwana kamkataa
Mke mwenza akiregea regea chuna chuna **buzi**
Ukiona mambo hayawezi kula kula vitu

Katika dondoo hilo, taswira buzi kama inavyoelezwa kwa kusema "Mke mwenza akiregea regea chuna buzi." inatumiwa na wanawake ili kumaanisha mwanamme ambaye yuko tayari kufanya ngono holela. Wanawake hasa wale wanaojiuza miili yao maarufu kama "mama poa" hapa Tanzania wamekuwa wakitumia neno "buzi" wakijisifia pale wanapopata mwanamme ambaye amekuwa akiwahudumia nje ya uhusiano wa ndoa kwa malipo ya ngono.

Katika wimbo wa ''*I love you baby''* pia kuna taswira ya kizuolojia pale muimbaji anapotumia neno la lugha ya Kiengereza "*baby*" lenye maana ya kamusi "mtoto." Usawiri wa taswira hii unajidhihirisha katika wimbo huo kama ifuatavyo:

Namba yako hii shikaaa
*I love you baby*
*I love you* ***baby***
*I love you baby*
*I love you baby*

Katika dondoo hilo, mwimbaji anatumia taswira pale anaposema "*I love you baby*." Matumizi ya neno "*baby*" katika ubeti huu yana lengo la kuonesha maana ya kimuktadha ambapo jamii imekuwa ikilitumia neno hili kwa maana ya mpenzi. Huu ni msimu ambao hutumiwa na wapendanao. Kutokana na matumizi ya neno hilo wahusika hujikuta wakiamini kwamba kuna mapenzi ya kweli katika uhusiano wao. Vile vile, neno "*baby*" hutumiwa kumaanisha "mtoto mdogo" au mtu ambaye ni mdogo ukilinganisha na mwenye rika kubwa.

Kwa upande wa wimbo wa *Full Stop* mtafiti amebaini kuwa kuna matumizi ya taswira ya neno "sharobaro" ambayo inaweza kuwekwa katika kategoria hii. Taswira

hii inaakisi vijana wa kisasa ambao wanapenda maisha ya anasa yakiwemo yale ya kufanya ngono holela. Kutokana na maisha hayo, vijana hao wanaonywa kuhusu tabia hiyo ambayo huweza kuwasababishia maambukizo hatari ya maradhi ya zinaa kama vile Ukimwi na ngono.

Tunaporejelea nadharia ya Simiotiki kwa kutumia msimbo wa Kiseme ambao unaangazia namna wahusika katika fasihi walivyoumbwa, ni wazi kuwa matumizi ya taswira za kizuolojia yaliyotumika katika nyimbo za Khadija Kopa yasawiri ishara ya wanajamii katika ulimwengu wa uhalisia. Matumizi ya viumbe hawa yanatoa picha ambayo huwakilisha matabaka yaliomo katika jamii.

### 4.2.1 Taswira za Botania

Hii ni taswira inahusu taswira ambazo zimejengwa kutokana na mimiea mbalimbali (Wamitila, 2003). Data zilizokusanywa na mtafiti zinaonesha kuwa baadhi ya nyimbo za Khadija Kopa zimekuwa zikitumia aina hii ya taswira. Taswira hizo zinajidhihirisha katika jadwali Na. 2 kama ifuatavyo:

**Jadwali Na. 4.1.2 Taswira za Botania katika Nyimbo za Khadija Kopa**

| **Na. ya Nyimbo** | **Jina la Nyimbo** | **Taswira** | **Maana** |
|---|---|---|---|
| 3 | Mwanamke Mambo | Fenesi | Kufanya ngono |
| 5 | *Full Stop* | Mizizi | Historia |

**Chanzo: Data za Utafiti Kutoka Nyimbo za Taarab za Khadija Kopa, Aprili, 2020**

Katika jadwali Na. 4.1.2 hapo juu data zinaonesha namna taswira za botania ambazo hujengwa kutokana na jamii ya mimea zinavyojidhihirisha katika nyimbo za taarab za Khadija Kopa. Kwa mfano, katika wimbo *Mwanamke Mambo* kuna matumizi ya

neno “fenesi” ambalo ni tunda kubwa la mfenesi lenye umbo refu na duara, utomvu mwingi na maganda linapopasuliwa na lina nduindui zinazochoma. Taswira hiyo inaelezwa hivi:

> Eee mwanamke raha ngoma namtikisia
> Kalipasua **fenesi** ee kalipasua
> Kalipasua fenesi ee kalipasua
> Kalipasua fenesi ee kalipasua

Katika ubeti wa hapo juu, taswira ya “fenesi” inatupatia picha ya kitendo cha kufanya maingiliano ya kimwili. Hivyo, kutokana na matumizi haya ya taswira ya fenesi muimbaji ametumia tafsida ili kuepuka kuzungumzia masuala ya maingiliano ya kimwili wazi wazi. Kwa ujumla matumizi haya yanasukumwa na mila na desturi za jamii ya Waswahili kutokana na mwiko wa kueleza masuala ya ngono kwa lugha ya wazi. Aidha, katika wimbo wa *Full Stop* kuna matumizi ya taswira ya botania yakiwakilishwa na neno “mizizi,” kama yanavyojidhihirisha katika beti ifuatayo:

> Mnaingilia mapenzi tunayopeana na bwana
> Nikianza na **mizizi** penzi si la mwaka janaa oooo
> Hatukuingia juzi juzi aaa jiji la Dar-es-salam

Katika dondoo hilo, kuna matumizi ya neno “mizizi” ambalo linatupa picha ya namna penzi linalozungumziwa lilivyoanza zamani na hivyo penzi hilo haliwezi kuvunjwa kwa urahisi. Ndio maana mtunzi anatueleza kuwa “Nikianza na mizizi penzi si la mwaka jana…” Kwa ujumla matumizi ya taswira ya botania katika nyimbo za Khadija Kopa sio makubwa yakilinganishwa na taswira nyengine.

Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki, hasa mhimili wa Kiishara, mtafiti amebaini kuwa nyimbo za Khadija Kopa zimetumia vitu kama vile fenesi na mizizi ili kusawiri dhana muhimu kama suala la mapenzi linazoihusu jamii. Kutokana na ishara hizo

zinawafanya wasikilizaji wa nyimbo hizo wazisikilize na kupata picha halisi zinazojengwa na taswira hizo ili kupata ujumbe uliokusudiwa.

### 4.2.2 Taswira za Kiastromia

Hii ni aina ya taswira ambazo hujengwa kutokana na vitu ambavyo hutoa mwanga na kumeremeta kama jua, mwezi, nyota na kadhalika. Katika nyimbo za Khadija Kopa, data zinaonesha kuwa kuna matumizi ya mbinu hii ya taswira ya kiastomia kama inavyojidhihirisha katika jadwali Na.4.1. 3 la hapo chini:

**Jadwali Na. 4.1. 3Taswira za Kiastromia za Khadija Kopa**

| Na. ya Nyimbo | Jina la Nyimbo | Taswira | Maana |
|---|---|---|---|
| 3 | Mwanamke Mambo | Jicho | Macho mazuri |
| 5 | *Full Stop* | Moto | Kufanya ngono holela. |
| | | Joto | Mapenzi |

**Chanzo: Data za Utafiti Kutoka Nyimbo za Taarab za Khadija Kopa, Aprili, 2020**

Katika jadwali Na. 3 hapo juu, mtafiti amebainisha data za utafiti ambapo katika wimbo *Mwanamke Mambo* kuna matumizi ya taswira ya “jicho” ambayo ina maana ya kiungo cha mwili katika uso wa kiumbe hai anachotumia kuonea (BAKIZA, 2010). Kwa kutumia taswira hii msikilizaji hupata picha ya namna mvuto wa mwanamke unavyoweza kuwa bora kutokana na uzuri wa macho yake. Kwa mfano, tunaelezwa hivi:

Eee mwanamke mambo
Eee mwanamke **jicho**
Ee mwanamke mambo

Katika dondoo hilo, tunaona namna mwimbaji anavyoona kuwa thamani ama uzuri wa mwanamke unavyokuwepo kutokana na uzuri wa macho yake. Tunapoelezwa

“Eee mwanamke jicho” ni taswira ambayo ni msimu katika jamii inayotumia lugha ya Kiswahili hapa Tanzania ambapo hutumiwa na wanawake ili kusifia uzuri wa mwanamke. Hata hivyo, ikumbukwe kuwa taswira hiyo hujengwa kwa kutumia neno “jicho” na si “macho.” Taswira nyengine ya kiastromia inapatikana katika wimbo wa *Full Stop* kama ifuatavyo:

Hatukuingia juzi juzi aaa jiji la dar-es-salam
Tumelifanyia kazi tukashusha na vilima
Tumeyafika mapenzi joto **joto** lazizima

Katika ubeti huo kuna neno “joto” ambalo linatupa picha ya namna hali ya mapenzi ilivyo ya kuridhisha. Anaposema “Tumeyafika mapenzi joto joto lazizima” mwimbaji anaonesha kuwa mapenzi yao yamefika kileleni na hayawezi kuathiriwa na kitu chochote. Aidha, katika wimbo huo wa *Full Stop* kuna matumizi ya taswira ya “moto,” ambayo ni miale mekundu inayounguza inayotokana na kitu kinachowaka (BAKIZA, 2010). Taswira hii imetumika ikiwa na maana ya kufanya ngono holela. Kitu kiunguapo na moto huteketea. Kwa maana hiyo,mwimbaji anasema ngono za kiholela humfanya mtu apate magonjwa kama vile ya Ukimwi na ngono ambayo huweza kuyateketeza maisha yake.

Mtafiti anaporejelea nadharia ya Simiotiki anagundua kwamba nyimbo za Khadija Kopa zinatumia ishara za kila aina ili kujenga taswira ambayo inamfanya ahisi kwa kutumia maneno hayo. Baadhi ya taswira hizo huteuliwa zikiwa na mwanga na huakisi utamaduni wa jamii uliozoea kutumia taswira hizo. Ambapo kwa kutumia ishara hizo ndio ujumbe huwa unapatikana. Kwa mfano, anapozungumzia suala la Ukimwi anadokeza “moto” ili kuonesha athari ya tendo hilo.

### 4.2.3 Taswira za Kijiolojia

Taswira nyengine zilizotumika katika nyimbo za taarab za Khadija Kopa ni taswira za kijiolojia. Hizi ni taswira zinazohusu gamba la ardhi. Vitu vinavyoweza kuingizwa katika aina hii ya taswira ni pamoja na miamba, madini, vitu vya shaba, bati, chuma, dhahabu, almasi na vito (Wamitila, 2004). Matumizi haya ya taswira ya kijiolojia yanajidhihirisha kama ifuatavyo:

**Jadwali Na. 4.1.4 Taswira za Kijiolojia katika Nyimbo za Khadija Kopa**

| Na. ya Nyimbo | Jina la Nyimbo | Taswira | Maana |
|---|---|---|---|
| 1 | Mwanamke Mambo | Kivumbi | Mapambano |
| 2 | *I Love You* | Dunia | Ulimwenguni |

**Chanzo: Data za Utafiti katika Nyimbo za Khadija Kopa, Aprili, 2020**

Jadwali Na. 4 hapo juu linaonesha namna nyimbo za Khadija Kopa zinavyotumia taswira ya kijiolojia kama sehemu ya kipengele cha fani. Katika wimbo wa *Mwanamke Mambo* kuna matumizi ya taswira inayojengwa kwa kutumia neno "kivumbi," kama inavyojidhihirisha katika ubeti ufuatao:

Kitatimka **kivumbi**
Kivumbi kitatimka kivumbi
Chumbani ukimfungia
Chumbani ukimfungia

Katika ubeti wa hapo juu, taswira ya kivumbi inatupatia picha ya vurugu, machafuko ama mgogoro utakaotokea pale mwanamme atakapozuiwa kwa kufungiwa chumba. Vile vile, katika wimbo wa *I Love You* kuna matumizi ya taswira ya kijiolojia inayojengwa kwenye neno "dunia" Taswira hiyo inajidhihirisha kama ifuatavyo:

Usihofu mpenzi wangu
Na wao tuwadharau

Usijali *baby* wangu
Na yao tuyasahau
Tupendane tupendane
Hadi yauumul-kiama
Tupendane tupendane
Hadi mwisho wa **dunia**

Katika ubeti huo tunaona namna msanii anavyotumia taswira ya dunia yenye maana ya maisha ya hapa ulimwenguni. Picha inayopatikana katika taswira hii ni kwamba mapenzi yanayoelezwa na msanii hayatotenganishwa na yatadumu hadi pale wapendanao watapotenganishwa na kifo. Kwa ujumla uteuzi huu wa maneno ambayo yanatujengea taswira za kijiolojia yanalandana na nadharia ya Simiotiki kwenye msimbo wa kiurejelezi kutokana na uhalisia wa mapenzi ya wapendanao yasivyoweza kutenganishwa ispokuwa ni tanzia ya kifo.

### 4.2.4 Taswira za Kiteolojia

Hizi ni taswira za kizahania za kiimani. Katika utafiti huu, data zinaonesha kuwa katika nyimbo za Khadija Kopa kuna matumizi ya taswira za Kiteolojia kama ifuatavyo:

**Jadwali Na. 4.1.5 Taswira za Kiteolojia katika Nyimbo za Khadija Kopa**

| Na. ya Nyimbo | Jina la Nyimbo | Taswira | Maana |
|---|---|---|---|
| 1 | Niliwaze | Manani | Muungu |
| 2 | Nimmeridhi | Mizungu | Nguvu za kichawi |
| | | Majini | Viumbe vya kidhahinia vinavyotumiwa na baadhi ya wanadamu kudhuru watu. |
| | | Jalali | Muumbaji wa viumbe |
| | | Mungu | Muumbaji wa viumbe |
| 4 | I Love You | Yauumul-kiama | Siku ya kufufuliwa viumbe ili kulipwa hesabu za matendo yao |

**Chanzo: Data kutoka Nyimbo za Khadija Kopa, April, 2020**

Data zilizokusanywa na mtafiti zinaonesha kuwa Khadija Kopa amekuwa akitumia taswira zinazolenga kudokeza masuala ya kiimani. Kwa mfano, katika wimbo *Niliwaze* kuna matumizi ya neno “manani” ambalo lina maana ya Mwenyezi Mungu mmoja ambaye ndie muumba wa mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake. Taswira hii inajitokeza kama ifuatavyo:

> Nipendeze niliwaze ili niwe furahani
> Nitulize nipendeze penzi liwe na imani
> Mafisadi tuwabeze washindwe pita njiani
> Unibebe uniweze kwa nguvu zake **Manani**
> Niamini nijitangaze niwepo vikaoni
> Unibebe uniweze kwa nguvu zake **Manani**
> Niamini nijitangaze niwepo vikaoni

Katika ubeti huo hapo juu msanii anatumia taswira ya Manani iliyo na maana ya Mungu. Kwa kutumia taswira hiyo tunapata picha inayotuonesha namna Khadija Kopa alivyo na imani ya kwamba kila kitu muwezeshaji ni Mungu. Kutokana na imani hiyo hata mapenzi yake anaona kuwa yatafanikishwa kutokana na nguvu za Mungu.Vile vile, taswira ya kiteolojia imetumika katika wimbo wa *Nimemridhi* pale Khadija Kopa anapotumia neno “mizungu.” Hili ni neno lenye maana ya kutumia uchawi au nguvu za majini ili kufanikisha jambo fulani. Msanii anajenga taswira hii kama ifuatavyo:

> Kwa ridhaa yangu nimeridhia wala si **mizungu**
> Ni chaguo langu nimemchagua yumo moyoni mwangu
> Sitaki majunguu mlonipikia waja walimwengu…

Katika ubeti huo, mwimbaji anatuonesha kuwa amekubali mapenzi ya mwanamme wake na wala si kutokana na nguvu za kishirikina. Hii ni kusema kwamba, mapenzi aliyonayo hayakuchangizwa na nguvu za majini bali ni kutokana na upendo wake wa

kweli. Vile vile, taswira ya kiteolojia imetumika kwa kutumia maneno “Majini,” “Mungu” na “Jalali” kama inavyojidhihirisha katika beti zifuatazo:

**Majini** mizunguo mliyonuiaa muamuzi **Mungu**

Mapenzi ni raha hayana hirinzi siyaramlini
Nimmeridhi nae kaniridhi lawama zanini
Nampenda kweli kwake sijiwezi oo ya salaa
Kashifa sijali nalienzi penzi vumbi ladhimu

Nampenda kweli kwake sijiwezi oo by sweety
Kashfa sijali nalienzi penzi oo ya habiby

Bure kwenu ndoli mnajipa kazi ya kumwaga sumu
Bure kwenu ndoli mnajipa kazi ya kumwaga sumu
Namuomba **Jalali** atatuhifadhi mapenzi ya dongoo
Naamini **Jalali** atatuhifadhi mapenzi ya dongoo

Kwa mujibu wa BAKIZA (2010) wanaeleza kuwa jini ni kiumbe dhahania asiyeonekana aliyeumbwa kwa moto. Katika beti ya hapo juu, taswira ya “majini” imetumika kuonesha imani ya mtunzi kwamba majini hayawezi kumshinda Mungu. Ndio maana anatueleza kuwa “Majini mizinguo mliyonuiaa muamuzi Mungu.” Aidha, katika beti hizo kuna matumizi ya taswira “Mungu” na “Jalali.” Kwa ujumla neno Jalali linaelezwa na BAKIZA (2010) kuwa ni sifa moja ya Mwenyezi Mungu kuwa ni mwenye utukufu. Taswira ya Mungu na Jalali zinatupatia picha kwamba ndie mwenye kuweza kuyalinda mapenzi ya mwimbaji huyo.

Taswira za kiteolojia kama zilivyofafanuliwa katika sehemu hii zinalandana na msimbo wa Kiurejelezi unaopatikana katika nadharia ya Simiotiki. Msimbo huu unajengwa kutokana na viashiria vya utamaduni vinavyorejelewa katika kazi husika. Wamitila (2002) anasema kuwa, urejelezi huu huunda uhalisi mahususi kutokana na matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka kwa wasomaji na kwa njia hiyo kuipa kazi

fulani nguzo za kitamaduni. Hivyo basi, nguzo za kiutamaduni zinazoashiriwa katika nyimbo za Khadija Kopa ni kuhusu imani juu ya Mungu na nafasi ya mazinguo ambapo katika jamii wapo wanaofanya mizungu lakini wanaamini kuwa suala hilo haliwezi kushinda nguvu za Mungu.

### 4.2.5 Taswira za Vitu vya Kawaida

Hizi ni taswira ambazo hutengenezwa na binadamu kwa uwezo wake binafasi kama vile kiti, kitanda meza, jahazi, na vitu vyenginevyo vinavyofanana na hivyo ambavyo hutumika katika shughuli mbalimbali (Wamitila, 2004, na Taufiq, 2016). Katika utafiti huu, data zinaonesha kuwa nyimbo za Khadija Kopa zina matumizi makubwa ya taswira za kawaida kama zinavyojibainisha katika jadweli Na. 6 la hapo chini:

**Jadwali Na. 4.1.6Taswira za Vitu vya Kawida**

| Na. ya Nyimbo | Jina la Nyimbo | Taswira | Maana |
|---|---|---|---|
| 1 | Niliwaze | Njia | Sehemu inayopita watu na vyombo vya usafiri vya nchi kavu |
| 2 | Nimmeridhi | Hirinzi | Aina ya fungo lenye kutumika kama kinga, ngao au kudhuru wengine. |
| | | Vibati | Maneno ya mitaani |
| | | Sumu | Kitu kinachoua |
| | | Bomba | Mzuri |
| | | Ngoma | Mwili |
| 3 | Mwanamke Mambo | Nyumba | Ndoa |
| | | Mavitu | Mapenzi |
| | | Kitumbua | Sehemu viungo vya uzazi vya mwanamke |
| | | Dirisha | Thamani katika nyumba itumikayo kupitisha hewa na mwanga chumbani |
| | | Mpira | Kitendo cha kufanya ngono |
| | | Kikuba | Mapamboo ya jadi |

| Na. ya Nyimbo | Jina la Nyimbo | Taswira | Maana |
|---|---|---|---|
| | | | yanayotengezwa kwa mrehani na mkadi |
| | | Hina | Majani ya mhina yanayotumiwa na wanawake kujipamba kama vile piko |
| | | Udi | Mapambo yanayochomwa ili kutoa harufu nzuri |
| | | Boli | Mapenzi |
| | | Liwa | Kipande cha mti kinachotumiwa na wanawake kujipaka mwili wake ili kusafisha na kung`arisha ngozi. |
| | | Buti | Kuchukua mume wa mtu |
| | | Mpira | Mapenzi |
| | | Goli | Kufanya mapenzi |
| | | Mkorogo | Vipodozi vinavyochubua ngozi |
| 5 | Full Stop | Kikombe | Dawa ya jadi ya kutibu magonjwa |
| | | Mrija | Kifaa kinachotumika kuvutia kwa kutumia mdomo kimiminika kama vile maji, juisi au soda na kunywa |

**Chanzo: Data kutoka Nyimbo za Khadija Kopa, April, 2020**

Taswira nyengine iliyotumika katika nyimbo za Khadija Kopa ni taswira za vitu vya kawaida. Kwa kutumia taswira za vitu vya kawaida kitu kimoja hukiwakilisha kitu chengine. Kwa mfano, katika wimbo *Niliwaze* kuna matumizi ya taswira ya "njia." Taswira hii inajidhihirisha hivi:

Nipendeze niliwaze ili niwe furahani
Nitulize nipendeze penzi liwe na imani
Mafisadi tuwabeze washindwe pita **njiani**
Aaa mafisadi tuwabeze washindwe pita **njiani**
Unibebe uniweze kwa nguvu zake manani

Katika dondoo hilo, tunapatiwa taswira ya "njiani" pale msanii anaposema "Mafisadi tuwabeze washindwe pita *njiani*." Njia ni moja kati ya huduma ya kijamii ambayo

hutumiwa na watu ama vyombo vya usafiri kuenda sehemu moja na nyengine. Pia, inayopatikana katika sehemu hii ni kwamba wale wanaorudisha nyuma mapenzi hayo hawatoweza kupita njiani iwapo mpenzi wake atampendeza na kumliwaza.

Pia katika wimbo wa *Nimemridhi* kuna taswira ya "hirizi." Mutiso (2012) anaieleza hirizi kuwa hutengenezwa kutokana na mawe, majani, mbegu, pembe, kucha, nywele, meno, madini, viwakilishi vya maumbo ya mwanadamu, medali, senti, na kadhalika. Anaendelea kueleza kuwa hirizi inaaminika kuleta baraka, kulinda na kutibu. Kwa mtazamo huu Khadija Kopa haamini hirinzi kama anavyosema:

> Mapenzi ni raha hayana **hirinzi** siyaramlini
> Nimeridhia nae kaniridhi lawama zanini

Katika dondoo hilo, mtunzi anapoelza "Mapenzi ni raha hayana *hirizi* siyaamini" anatupatia picha ya kwamba mapenzi hayawezi kunogeshwa kwa kutumia hirizi. Mawazo haya ya Khadija Kopa yanayojidhihirisha katika dondoo hilo yanapingana na yale ya Mutiso (2012) ambaye anaeleza kuwa hirizi hutumiwa kukinga, kufanikisha na kuponyesha. Hivyo, maana tunayoipata kupitia taswira hii ni kwamba mapenzi hayawezi kufanikishwa kwa kutumia hirizi. Aidha, katika wimbo *Nimemridhi* kuna matumizi ya taswira ya "vibati" pale msanii anaposema "mpige vibati" ambayo inatupatia picha ya kueleza na kupigia kelele jambo fulani kwa lengo la kudhoofisha. Taswira hii inajitokeza hivi:

> Maneno mseme mpige **vibati** hata mkizua
> Na mtu hajanie baya halifiki mnajisumbuaa
> Na mtu hajanie baya halifiki mnajisumbuaa
> Nataka mseme penzi halitawaa

Taswira ya "kupiga vibati" kama inavyoelezwa katika dondoo hilo, mtunzi ameizalisha kutokana na antonemia ya "Kupiga debe" yenye maana ya kumtetea mtu

ili apate wafuasi wa kumuunga mkono juu ya suala fulani au apate jambo fulani. Kinyume chake ni kwamba taswira ya “mpige vibati” inamaana ya kwamba maneno yanayotolewa yanalenga kudhoofisha mapenzi yaliopo lakini kwa watu wanaopendana maneno hayo hayatadhoofisha penzi lao. Kwa maneno mengine Khadija Kopa anatueleza kuwa kelele za watu haziwezi kuvunja pendo la watu wanaopendana kwa dhati.

Taswira nyengine ya vitu vya kawaida iliyotumika katika nyimbo za Khadija Kopa ni matumizi ya neno “sumu” pale anaposema “Bureni kwenu ndoli mnajipa kazi ya kumwaga **sumu.”** BAKIZA (2010) wanaeleza kuwa sumu ni kemikali, dawa au kilichoharibika kinachodhuru au kuua. Picha inayopatikana kupitia taswira hii ni kwamba kuna watu ambao wanalenga kuharibu mafanikio yamapenzi ya mhusika. Vile vile, kuna taswira ya “bomba” na “ngoma” kama zinavyojidhihirisha katika beti ifuatayo:

Mwalilia wivu nimepata kitu **bomba** mie
Kazi kwenu wachovu sasa mambo yangu laivu mie
Mtoto bado nalipa na **ngoma** za uhakika
Mtoto naserebuka namwagia mahaba mie
Nna mkonu nyayoni maraha mpaka kichwani
Sasa mwalilia wivu nimepata kitu **bomba** mie
Zingatia mafundisho bibi alonifundisha

Katika dondoo la hapo juu neno “bomba” limetumika kumaanisha kitu kizuri. Hivyo Khadija Kopa anaposema “Mwalilia wivu nimepata kitu bomba mie” anamaana kwamba amepata mwanamme ambaye amemridhi. Aidha, kuna matumizi ya taswira “ngoma” pale anapoeleza “Mtoto bado nalipa na **ngoma** za uhakika.” Ngoma ni kifaa cha muziki kinachotengenezwa kwa mbao na kuvishwa ngozi ili kutumika

katika muziki. Picha tunayoipata hapa ni mapenzi ya dhati na yenye kumfanya mpenzi wake aridhike nayo.

Kwa upande wa wimbo wa *Mwanamke Mambo* kuna matumizi ya taswira ya "nyumba." Katika wimbo huo, neno nyumba limetumiwa kumaanisha "mwanamke aliye katika ndoa." Tazama matumizi ya taswira hii katika beti ifuatayo:

> Nitakutoa ushamba hataki nimemtenga
> Kama wewe mwenye **nyumba** ona mie kanitaka ooo kanitaka
> Kanitaka mwenyewe kanitaka
> Nishamsomba nishamsomba nitamchukua

Katika ubeti huo, taswira ya "nyumba" ambayo inapatikana katika mshororo wa pili unaosema "Kama wewe mwenye **nyumba** ona mie kanitaka ooo kanitaka." Neno "nyumba" kama lilivyotumika katika ubeti huo, lina maana ndoa. Katika jamii za Uswahilini hasa Visiwa vya Zanzibar wanandoa hulitumia neno "nyumba" ili kumaanisha uhusiano wa ndoa. Kutokana na maana hiyo ndio maana baadhi ya watu husema "usitake kunivunjia nyumba yangu" wakiwa na maana ya kukemea kuharibiwa uhusiano wa ndoa. Hii ni taswira ambayo inalengo la kushadadia dhamira ya mapenzi. Kupitia matumizi haya ya taswira tunakutana ukweli wa mawazo ya Wanyonyo (2015) pale anaposema kuwa baadhi ya taswira hutumika kutilia mkazo maudhui ya kazi husika.

Vile vile, Khadija Kopa katika wimbo wa *Mwanamke Mambo* ametumia taswira ya "mavitu" na "buti." Mavitu katika hali ya kawaida ni wingi wa vitu ambapo baadhi ya watu vitu vinapokuwa vingi sana hukengeusha mofolojia ya Kiswahili sanifu ya neno hilo na kusema "ma-vitu." Vile vile, neno buti katika wimbo huu limetumika

kwa maana ya "kushikilia kitu ili kisimtoke" Katika wimbo huu matumizi haya ya taswira yanajidhihirisha kama ifuatavyo:

Ukiona mambo hayawezi kula kula **vitu**
Ukiona kafunga funga kaza **buti**
Mpira ukiruswa nadaka
Mpira ukiruswa nadaka
Nafunga goli kwa tintaka
Karibu tapewa talaka

Katika beti hii, taswira ya "vitu" ina maana ya mapenzi. Hivyo tunapoambiwa kuwa "Ukiona mambo hayawezi kula vitu" picha inayopatikana ni ile ya kuhamasisha kufanya ngono ama kumchukulia mtu muume wake kutokana na udhaifu wa moja kati ya wapenzi husika. Mawazo haya yanaendelezwa kwa kutumia taswira ya "buti" pale msanii anaposema "Ukiona kafunga funga kaza buti." Ambapo tunapata picha ya kwamba iwapo mwanamke ataondoka kutokana na wivu basi hiyo ni furaha kwa mwanamke mwengine aliyemo katika ndoa ya mitara, cha muhimu ni kuzidisha mapenzi ili kudhibiti zaidi ndoa hiyo.

Pia, Khadija Kopa anaonekana amekuwa akitumia taswira zinazorejelea mapambo ya jadi ya wanawake wa Uswahilini ambao ni wanawake wanaoishi katika upwa wa Afrika Mashariki. Kwa mfano, katika wimbo wa *Mwanamke Mambo* kuna matumizi ya taswira ya "kikuba," "udi," "liwa," na "hina." Kwa mfano, anapohamasisha umuhimu wa kuweka sawa ngozi, Khadija Kopa anatumia taswira ya liwa na kusema "Mwanamake liwa mimi namsugua." Kwa ujumla taswira hizi zinajitokeza kama ifuatavyo:

Mwanamke **kikuba**
Mwanamke **hina**
Mwanamke **udi**
Mimi namfukizia

Matumizi ya taswira “kikuba,” “hina,” na “udi” kama yanavyojidhihirisha katika dondoo hilo yanatupatia picha ya msimamo alionao Khadija Kopa kuhusu mapambo ya wanawake. Mtazamo huu unalenga kuthamini mapambo ya jadi au asili ya Uswahilini na kudharau mapambo ya kisasa yanayotumiwa na wanawake ambayo yanachimbuko la tamaduni za Kimagharibi ndio maana katika wimbo huo anasema “Mie *beautiful nature* Sio mkorogo ulojipaka,” ambapo kwa kutumia taswira ya “mkorogo” yaani ngozi iliyobadilishwa kwa kutumia madawa na vipodozi vyenye kemikali, haina nafasi kwake. Mapambo ya jadi yanayopigiwa chapuo katika wimbo ni ishara ya kaida katika jamii za Waswahili. Wanyonyi (2015) anazieleza ishara za kaida kuwa ni ishara ambazo hujikita katika kabila fulani, kundi la watu au taifa husika. Anaendelea kueleza kuwa baadhi ya isahara za kaida zinaweza kuwa za kijadi kwa kuwa zinahistoria ndefu katika jamii husika na hujitokeza kama sehemu ya utamaduni wake. Hivyo picha inayopatikana kupitia taswira hizi ni kwamba ingawa jamii hiyo imekumbwa na utandawazi wa kutumia mapambo ya Kimagharibi, utamaduni wa mapambo ya jadi unaendelea kuthaminiwa.

Vile vile, kuna matumizi ya taswira ya neno “ngoma.” Kwa mujibu wa BAKIZA (2010) ngoma ni kifaa cha muziki ambacho kinawambwa kwa ngozi. Kwa kutumia kifaa hiki Khadija Kopa ametuchorea taswira kama inavyojidhihirisha katika ubeti ufuatao:

Ee mwanamke raha **ngoma** namtikisia
Unaenda sijigonge gonge nitajivua weyee
Tutakula kwa matonge sambamba tutatumia
Ukiumwa kajigonge weye
Ukiumwa kajigonge weye

Taswira ya "ngoma" kama inavyojidhihirisha katika dondoo hilo ina maana ya mwili ama kiuno katika miktadha ya mapenzi. Taswira hiyo inatupatia picha ya namna msemaji alivyoridhika na penzi lao. Khadija Kopa amefungwa na miiko ya kijamii ya kuzungumzia kitendo cha kufanya mapenzi kwa lugha ya kawaida. Hivyo ili kulinda miiko hiyo ameamua kutumia neno ngoma. Uteuzi huu wa matumizi ya lugha ya kitaswira kwa kutumia maneno ya kawaida ni sifa moja wapo ya taswira kama anavyoeleza Khamis (2004) kwamba miongoni mwa sifa mbalimbali za taswira ni kwamba zinaweza kuundwa na lugha ya kawaida au ya kitamathali, kujitokeza katika umbo sahihi au changamani, kuwepo kwa taswira nyororo au nzito na zile za asili au za kukopwa.

Vile vile, Khadija Kopa anatumia taswira zilizojengwa kwa kutumia majengo. Katika wimbo wa *Mwanamke Mambo* kuna taswira za "chumba" na "dirisha." Kupitia taswira hizo tunapata picha ya namna msanii alivyokusudia kuhakikisha amempata yule anayemtaka kufanya naye mapenzi bila kujali kuwa ni muume wa mtu. Taswira hizi zinajibainisha kama ifuatavyo:

> **Chumbani** ukimfungia
> Nitamuinda kama paka
> Nitamuinda kama paka
> **Dirishan**i nitamtoa
> Sitishwi nikitishika
> Raha zimenikolea

Katika beti hizo hapo juu, msanii anaposema "Chumbani ukimfungia…Dirishani nitamtoa" picha inayopatikana ni kwamba kutokana na mapenzi aliyonayo anaweza kufanya lolote au kutumia mbinu yoyote ili kufanikisha utashi wake wa mapenzi. Suala la wivu ambalo linaweza kumfanya mwanamme adhibitiwe ndani na

mwanamke hilo anaona kuwa bado si kikwazo cha kutofanikisha mpango alionao wa kumpata anayemtaka.

Matumizi mengine ya taswira katika nyimbo za Khadija Kopa yamejengwa kwa kutumia miktadha ya viwanja vya michezo. Katika wimbo wa Mwanamke Mambo msanii anatumia taswira ya "mpira" na "goli" kama taswira hizo zinavyojidhihirisha katika beti zifuatazo:

Sio mkorogo ulojipaka
Sio mkorogo ulojipaka
**Mpira** ukirushwa nadaka
**Mpira** ukirushwa nadaka
Nafunga goli kwa tiktaka
Karibu tapewa talaka

Mpira ukiruswa nadaka
Nafunga **goli** kwa tiktaka
Karibu tapewa talaka

Katika beti hizo, Khadija Kopa anaonekana akitumia taswira ya "mpira" na "goli" ili kusawiri mapenzi. Katika beti hizi msanii anaposema "Mpira ukirushwa nadaka" picha inayopatikana na kwamba mpenzi wake anapotaka kufanya mapenzi anakuwa tayari kwa tendo hilo. Aidha, msanii anaposema "Nafunga goli kwa tikitaka" anamaana kwamba amekuwa akimridhisha mpenzi wake kutumia njia mbalimbali ili kufanikisha mapenzi hayo. Aidha, katika wimbo wa *Full Stop* Khadija kopa anatumia taswira ya "kikombe" na "mrija" kama inavyojidhihirisha katika ubeti ufuatao:

Loliondo kwa babu
Sharobaro kapewa **kikombe**
Akasema nangoja **mrija** mie

Katika dondoo hilo, taswira ya "kikombe" ambacho kimehusishwa na Loliondo kwa babu imetumika ili kusawiri matumizi ya dawa za kienyeji katika kutibu magonjwa mbalimbali ikiwemo Ukimwi. Vile vile, taswira ya "mrija" inatupatia picha ya namna inavyotumika dawa hiyo. Picha inayopatikana kutokana na taswira hii ni kwamba Khadija Kopa haamini matumizi ya dawa ya jadi maarufu kama "kikombe cha babu" iliyowahi kutokea huko Tanzania ikiaminiwa kuwa inatibu magonjwa yote. Kutokana na mtazamo alionao Khadija Kopa kutokana na dawa hiyo ndio maana anasema "Sharobaro kapewa kikombe, akasema nangoja mrija mie." Hii ni kejeli inayolenga kuwatahadharisha vijana baada ya kupata magonjwa. Kwa upande mwengine tunaweza kusema kuwa picha inayopatikana katika taswira hii ni namna vijana amabao wanajiingiza katika ngono wanavyoweza kujikuta wakishindwa kufanya mapenzi kwa sababu ya magonjwa. Kwa kutumia mtazamo huu "kikombe" kinakuwa mwanamke na mrija "nguvu za kiume." Kungoja mrija inaashiria kijana kutaka kusubiri kutokana na athari za kupoteza nguvu kutokana na ugonjwa.

Kwa ujumla matumizi ya taswira za vitu vya kawaida ni makubwa inapolinganishwa na aina nyengine za taswira katiika nyimbo za Khadija Kopa. Matumizi haya ya vitu vya kawaida yanalandana na nadharia ya Simiotiki katika msimbo wa Ki-ishara. Kwa mujibua wa Wamitila (2002) msimbo huu unahusishwa na jinsi ambavyo wasomaji wanavyovumbua maana mbalimbali za ki-ishara katika kazi ya kifasihi. Hivyo kwa kutumia vitu vya kawaida vinavyotengenezwa na wanajamii husika msanii amefanikiwa kujenga taswira zake na hatimae kuiakisi jamii katika nyanja mbalimbali za maisha hususani mapenzi.

## 4.3 Miktadha ya Matumizi ya Taswira katika Nyimbo za Taarabu za Khadija Kopa

Lengo mahususi la pili la utafiti huu lilikuwa ni kutaka kubainisha miktadha ya matumizi ya taswira katika nyimbo za mapenzi za Khadija Kopa. Ili kulifikia lengo hilo, mtafiti alizikusanya data na kuzitalii kwa mbinu ya usomaji makini huku akidondoa data za taswira na namna zilivyotumika katika miktadha mbalimbali. Kwa ujumla, data hizo zilionesha kuwa Khadija Kopa amekuwa akitumia taswira katika miktadha ya kiutamaduni, mapenzi, magonjwa ya zinaa, utandawazi na miktadha ya kifasihi. Hivyo basi, katika sehemu hii miktadha hiyo imebainishwa kama ifuatavyo:

### 4.3.1 Miktadha ya Mapenzi

Kwa mujibu wa BAKIZA (2010) mapenzi ni hisia nzito ya moyoni inayomfanya mtu avutiwe, athamini na ajali mtu au jambo. Visawe vya mapenzi ni pamoja na mahaba au huba. Miktadha ya mapenzi ni moja kati ya miktadha iliyomsukuma Khadija Kopa kutumia taswira katika nyimbo zake. Kwa mfano, katikata wimbo wa *I love you* Khadija Kopa ametumia taswira ya kizuolojia ya neno la lugha ya Kiengereza "baby," ili kuonesha mapenzi ya dhati. Matumizi ya neno hilo yamejitokeza kama inavyoonekana katika beti ifuatayo:

Namba yako hii shikaaa
*I love you* ***baby***
*I love you* ***baby***
*I love you* ***baby***
*I love you* ***baby***

Katika dondoo hilo, muimbaji anatumia taswira pale anaposema "*I love you baby*." Matumizi ya neno "baby" katika ubeti huu limetumika ili kusawiri muktadha wa mapenzi. Ni kawaida ya Waswahili wengi kuonesha hisia zao za mapenzi kwa

kutumia mchanganyo ndimi ambapo ili kushadidia na kuthibitisha hisia zao za mapenzi kwa yule wanayempenda wamekuwa wakitumia neno “baby.” Matumizi ya neno hili ni kama vile kwamba wapendanao wanaweza kusaidiana kwa hali yoyote kama wanavyofanya kwa watoto. Vile vile, kuna taswira ya neno “mpenzi” katika beti inayosema:

> usihofu **mpenzi** wangu
> na wao tuwadharau
> usijali baby wangu
> na yao tuyasahau
> tupendane tupendane

Katika beti hii, taswira ya neno “mpenzi” imejengwa ili kukidhi mawasiliano yanayohusu muktadha wa mapenzi. Kutokana na miktadha ya mapenzi mwimbaji anaeleza “usihofu mpenzi wangu.” Haya ni mazungumzo ambayo yanalenga kujenga uhusiano wa mapenzi kati ya wahusika. Miktadha mengie ya matumizi ya taswira yanayosukumwa na miktadha ya mapenzi yanajitokeza katika wimbo wa *Full Stop* pale mtunzi anapotumia neno “joto” kama inavyoonekana katika mfano ufuatao:

> Hatukuingia juzi juzi aaa jiji la Dar-es-salam
> Tumelifanyika kazi tukashusha na vilima
> Tumeyafika mapenzi joto **joto** lazizima

Taswira ya neno “joto” iliyotumika katika ubeti huu limetumika katika dondoo hilo imetumika ili kuonesha namna msanii anavyoonesha kuridhika na mapenzi ambayo yamekuwapo kati yao. Anajaribu kusawiri maisha halisi ya jiji la Dar es Salam huko Tanzania ambako katika jiji hilo wanawake wengi wamekuwa wakiamini kuwa ni wajuzi wa kufanya mapenzi.

Kinachoonekana kupitia taswira hizi ni kwamba Khadija Kopa anasawiri miktadha ya mapenzi ili kuiburudisha hadhira yake. Kama anavyoeleza Otieno (2017) kwamba

nyimbo za mapenzi hutumika ili kuonesha hisia za mahaba kati ya wapenzi wawili. Hivyo basi, taswira hizo zimetumika ili kudhihirisha mahaba hayo. Taswira hizo zinalandana na nadharia ya Simiotiki katika msimbo wa Kiurejelezi ni kwamba taswira zilizotumika zinaakisi maneno ya mahaba yanayotumiwa na wanajamii wakati wa kudhihirisha mapenzi yao.

### 4.3.2 Miktadha ya Utamaduni

Miktadha mingine ambayo inamsukuma Khadija Kopa kutumia taswira katika nyimbo zake za mahaba ni miktadha ya utamaduni. Utamaduni ni jumla ya mila na desturi zinazofuatwa na wanajamii. Data zilizokusanywa na mtafiti zinaonesha kuwa katika wimbo wa *Mwanamke Mambo* kuna matumizi ya taswira ya "fenesi." Kwa mujibu wa BAKIZA (2010) fenesi ni tunda kubwa la mfenesi lenye umbo refu na duaradufu, utomvu mwingi na maganda linapopasuliwa na lina ndui ndui zinazochoma. Taswira hii inasawiriwa kamaifuatavyo:

Eee mwanamke raha ngoma namtikisia
Kalipasua **fenesi** ee kalipasua
Kalipasua fenesi ee kalipasua
Kalipasua fenesi ee kalipasua

Taswira ya "fenesi" kama inavyojidhihisrisha katika ubeti wa hapo juu inalenga kueleza kuwa anayezungumziwa amekuwa akifanya ngono. Mwimbaji ametumia taswira hii ili kuepuka matumizi ya lugha ya wazi wakati wa kuelezea maingiliano ya kimwili ambayo ni karaha kuzungumza suala hilo wazi wazi kwa utamaduni wa Uswahilini na Afrika kwa ujumla.Vile vile, katika wimbo wa *Mwanamke Mambo* kuna matumizi ya taswira ya "jicho" ambayo ina maana ya mwanamke mrembo. Taswira hii inajibainisha katika ubeti ufuatao:

Eee mwanamke mambo
Eee mwanamke **jicho**
Ee mwanamke mambo

Katika dondoo hilo, tunaona namna taswira ya jicho inavyotumika kumsifia mwanamke kutokana na uzuri wake pale mwimbaji anaposem "Eee mwanamke jicho." Katika jamii ya Tanzania ni utamaduni wa wanawake wengi kujiremba macho kama sehemu muhimu ya kumfanya mwanamke avutie. Wanawake wamekuwa wakijipamba macho yao kwa kutumia wanja na vipambo vyengine ikiwa ni pamoja na kubandika kope. Hili hufanywa na wanawake ili kuwa na mvuto wa macho yao.

Vile vile, kuna taswira ya "bomba" na "ngoma" kama zinavyojidhihirisha katika beti ifuatayo:

Mwalilia wivu nimepata kitu **bomba** mie
Kazi kwenu wachovu sasa mambo yangu laivu mie
Mtoto bado nalipa na **ngoma** za uhakika
Mtoto naserebuka namwagia mahaba mie
Nna mkuna nyayoni maraha mpaka kichwani
Sasa mwalilia wivu nimepata kitu **bomba** mie
Zingatia mafundisho bibi alonifundisha

Katika dondoo la hapo juu taswira inayojengwa katika neno "bomba" ambalo kwa mujibu wa BAKIZA (2010) neno hilo linamaana changamano ambazo ni; chombo cha kupazia sauti, paipu pana kwa ajili ya kusafirishia kitu kirowevu, sehemu ya juu katika jengo au chombo cha baharini maalumu kwa kutolea moshi, kifaa ambacho kinatumiwa kudungia sindano na kifaa kinachotiwa dawa na kupulizwa ili kuua wadudu kama vile mbu. Katika ubeti huo maana za kamusi kama zilivyobainishwa hapo juu zinakengeushwa na kupewa maana ya ziada na kuwa maana ya "mzuri." Aidha, neno hilo hutumika ili kumaanisha mtu aliye na mvuto katika kufanya

mapenzi. Hivyo Khadija Kopa anaposema "Mwalilia wivu nimepata kitu bomba mie" anamaana kwamba amepata mwanamme mzuri ambaye amemridhia. Matumizi haya ya neno "bomba" yana lengo la kulinda miiko na maadili ya utamaduni wa Mswahili ambayo hauruhusu kuzungumzia masuala ya mahusiano ya mapenzi waziwazi.

Aidha, taswira "ngoma" inayopatikana katika msitari wa tatu wa beti ya hapo juu unaosema "Mtoto bado nalipa na **ngoma** za uhakika." Miktadha ya kiutamaduni ndio iliyomsukuma msanii kutumia taswira hizo kutokana na kwamba katika neno **ngoma** na neno **bomb**a yana tupatia picha ya harakati za kufanya mapenzi kitendo ambacho ni miiko kukizungumza mbele ya hadhira kwa lugha ya kawaida.

Kwa upande wa wimbo wa *Mwanamke Mambo* kuna matumizi ya taswira "nyumba." Katika wimbo huo, neno nyumba imetumiwa kumaanisha "mwanamke aliye katika ndoa." Taswira hii inajidhihirisha kama ifuatavyo:

> Nitakutoa ushamba hataki nimemtenga
> Kama wewe mwenye **nyumba** ona mie kanitaka ooo kanitaka
> Kanitaka mwenyewe kanitaka
> Nishamsomba nishamsomba nitamchukua

Katika dondoo hilo taswira ya nyumba iliyo na maana ya mwanamke aliyemo katika ndoa imetumika ili kufuata taratibu na kanuni za utamaduni wa jamii za Uswahilini hasa huko katika visiwa vya Zanzibar ambako ni mwiko kumtaja wazi wazi mtu mkewe. Hivyo ili kuepuka miiko hiyo watu hutumia neno "nyumba" kama inavyojidhihirisha katika ubeti huu msanii anaposema "Kama wewe mwenye **nyumba** ona mie kanitaka ooo kanitaka." Kwa ujumla katika jamii za Uswahilini ni

kawaida ya mwanamme kusikia akisema kuwa "wataka kunivunjia nyumba yangu," akiwa na maana kuwa ataka kuvunja ndoa kati yake na mke wake.

Miktadha ya kiutamaduni pia imetumika katika wimbo wa *Mwanamke Mambo*. Katika wimbo huo mtunzi ametumia taswira ya "mavitu" na "buti." Taswira ya mavitu imetumika ili kutoa picha ya kitendo cha kufanya gono. Vile vile, "buti" ni taswira iliyotumika kutoa picha ya kumnyang`anya mwanamke mume aliyenaye na kumchukua kufanya naye mapenzi. Matumizi haya ya maneno kama taswira nyengine zilizokwisha elezwa katika sehemu hii ni kwamba zimetumiwa na msanii ili kupunguza ukali wa maneno ambayo huweza kuleta karaha miongoni mwa hadhira. Hii ni kwa sababu katika jamii ya Tanzania kuzungumzia suala la mapenzi yanayohusu maingiliano ya mwili hutakiwa liwe na ubanifu wa kimafumbo.

Pia, data zilizokusanywa na mtafiti zinaonesha kuwa Khadija Kopa ametumia taswira zinazolenga kusawiri miktadha ya utamaduni inayohusu mapambo ya jadi. Mapambo hayo yanaelezwa kwa taswira ya "kikuba," "udi," "liwa," na "hina." Kwa ujumla taswira hizi zinajitokeza kama ifuatavyo:

Mwanamke **kikuba**
Mwanamke **hina**
Mwanamke **udi**
Mimi namfukizia

Matumizi ya taswira "kikuba," "hina," na "udi" kama yanavyojidhihirisha katika dondoo hili yanatupatia picha ya miktadha ya jadi ya wanawake wa Uswahilini ambao wamekuwa wakitumia vitu hivyo katika mapambo yao. Mulokozi (1999) anamueleza Binti Mshamu, mwanamke wa Uswahilini katika *Utenzi wa Mwana Kupona* namna anavyomuusia Mwanakupona kutumia hina na vitu vyengine vya jadi

ili kujipamba kwa ajili ya usafi wa mwili ambao utafanya mvuto mbele ya mume wake.

Vile vile, kuna matumizi ya taswira ya inayojengwa kwa kutumia neno “ngoma,” ambalo linasawiri miktadha ya utamaduni wa Watanzania. Ingawa BAKIZA (2010) wanalifasiri neno “ngoma” kuwa ni kifaa cha muziki ambacho kinawambwa kwa ngozi. Kwa kutumia kifaa hiki Khadija Kopa anasawiri miktadha ya utamaduni wa jamii iliyomkuza kama ifuatavyo:

Ee mwanamke raha **ngoma** namtikisia
Unaenda sijigonge gonge nitakuvua weyee
Tutakula kwa matonge sambamba tutatumia
Ukiumwa kajigonge weye
Ukiumwa kajigonge weye

Taswira ya “ngoma” iliyomo katika mshororo wa kwanza wa ubeti huu unaosema “Ee mwanamke raha ngoma namtikisia” Hii ni taswira inayotumika ili kusawiri utamaduni wa jamii. Picha inayopatikana hapa inasawiri harakati za kufanya mapenzi namna mhusika anavyotingisha mwili wake. Maana hii inapatikana kwa kuzingatia miktadha ya matumizi ya lugha. Mawazo haya yanaungwa mkono na Carston na Powell (2006) ambao wanaeleza kuwa ili kutambua maana ya kauli fulani lazima kuzingatiwe muktadha wa mawasiliano hayo. Hii ni kwa sababu neno fulani huweza kutoa maana tofauti iwapo litatumika katika miktadha tofauti. Kwa ujumla tunaporejelea nadharia ya Simiotiki kwa kutumia msimbo wa Kiishara ni kwamba taswira katika nyimbo za Khadija Kopa zimetumika ili kutunza utamaduni wa jamii ya msanii huyo.

Kwa ujumla taswira zilizotumika katika sehemu hii zinalandana na msimbo wa Kiurejelezi wa nadharia ya Simiotiki. Hii ni kutokana na kwamba msimbo huu

unajengwa kutokana na viashiria vya utamaduni unaorejelewa katika kazi inayohusika. Urejeshi huu huunda uhalisi mahususi kutokana na matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji na kwa njia hiyo huipa kazi fulani nguzo kitamaduni (Wamitila, 2002). Hivyo basi, taswira zilizobainishwa katika sehemu hii zinajikita kutii miiko ya utamaduni au kiashiria cha utamaduni wa Mswahili.

#### 4.3.3 Miktadha ya Utandawazi

Utandawazi ni sera ambayo inaufanya ulimwengu kuwa kama kijiji. Kwa kutumia sera ya utandawazi dunia inajikuta ikiwa na maingiliano makubwa ya utamaduni, biashara, siasa na mambo mengine yakijamii. Miktadha ya utandawazi imemsukuma Khadija Kopa kutumia taswira. Kwa mfano, katika wimbo wa *Mwanamke Mambo* kuna taswira “buzi.” Taswira hii inatupatia picha ya wanawake kufanya ngono holela. Hivyo taswira hii inaelezwa hivi:

> Lipi anataka msaada na bwana kamkataa
> Mke mwenza akiregea regea chuna chuna **buzi**
> Ukiona mambo hayawezi kula kula vitu

Katika dondoo hilo, taswira buzi kama inavyoelezwa kwa kusema “Mke mwenza akiregea regea chuna buzi.” taswira hii imekuwa ikitumiwa na wanawake wa kisasa ambao wamekuwa wakifanya ngono kama mtaji wao. Wanawake hao hujiuza bila ya kujali miiko ya kidini wala utamaduni. Hili ni tapo la wanaufemisti wa msimamo mkali kama wanavyoelezwa na Wamitila (2003) ambaye analieleza kundi hilo kuwa ni wanawake ambao wamekuwa na msimamo mkali wa kutaka uhuru wa kufanya kila wanalolitaka bila ya kuzuiwa na vikwazo vya kiutamaduni. Hivyo, uhamasishaji huu wa kufanya ngono holela unaweza kuwekwa kama moja ya athari ya tapo hilo ambalo limekita ulimwenguni hasa katika nchi za Magharibi.

Vile vile, katika wimbo wa *Full Stop* kuna matumizi ya taswira ya “masharobaro” linalosawiriwa katika miktadha hii ya utandawazi. Neno masaharobaro hutumika likiwa na maana ya vijana wa kiume ambao ni watanashati na wamekuwa wakifuata tamaduni za Kimagharibi katika maisha yao kama vile kuiga mavazi ya Kimagharibi, muziki na hata kupenda kufanya ngono na mwanamke yoyote wanayevutiwa naye. Kutokana na tabia hiyo Khadija Kopa anatumia taswira ya “moto” ambapo anatupatia picha ya ngono holela. Tazama mfano ufuatao:

Mtoto wangu wa kiume nisikilizeni
Mnaojiita masharobaro nisikilizeni
Nyie mabarobaro nisikilizeni
Nawambia kina kaka wanawake wanajua
Pale panapo utamu wamepapamba maua
Ukikosa gonoria Ukimwi utakuuwa
Ukimwi utakuuwa
Ukimwi utakuuwa
Eee usiguse moto utakuunguza
Eee usiguse moto utakuunguza

Katika ubeti huo tunaona namna matumizi ya taswira “Mnaojiita masharobaro nisikilizeni” inavyolenga kusawiri na kuwaonya vijana hao wanaojiita masharobaro kuhusu suala la kufanya ngono holela. Vijana hao wanatakiwa wajuwe kuwa wanawake wamekuwa na tabia ya kufanya mvuto wa wanaume kutokana na kujiremba ndio maana katika wimbo huo tunaelezwa kuwa “Nawambia kina kaka wanawake wanajua, Pale panapoutamu wamepapamba maua.” Hivyo iwapo wataendeleza tabia ya ngono holela athari zake ni mbaya ikiwa ni pamoja na kupatwa na magonjwa ya Ukimwi na hata gono.Kwa kutumia nadharia ya Simiotiki

tunaona kuwa taswira ya "buzi" na "sharobaro" ni viashiria ambavyo vinaonesha tabia ya kuiga utandawazi katika jamii.

### 4.3.4 Miktadha ya Imani

Dini ni mfumo mzima wa maisha ya mwanadamu. Data zilizokusanywa na mtafiti zinaonesha kuwa Khadija Kopa amekuwa akitumia taswira zinazosawiri miktadha ya imani ya dini ambayo inalenga kuamini kuwepo kwa Mwenyezi Mungu na kwamba yeye ana uwezo wa kumsaidia kiumbe wake. Kwa mfano, katika wimbo *Niliwaze* kuna matumizi ya taswira "Manani" ambayo inatupa maana ya Mwenyezi Mungu mmoja ambaye ndie muumba wa mbingu na ardhi na viliomo ndani yake. Taswira hii inajitokeza kama ifuatavyo:

Nipende niliwaze ili niwe furahani
Nitulize nipendeze penzi liwe na imani
Mafisadi tuwabeze washindwe pita njiani
Aaa mafisadi tuwabeze washindwe pita njiani
Unibebe uniweze kwa nguvu zake **Manani**
Niamini nijitangaze iwepo vikaoni
Unibebe uniweze kwa nguvu zake **Manani**
Niamini nijitangaze kwa nguvu zake **Manani**.

Katika beti hii tunaona namana mtunzi anavyotumia taswira ya kiteolojia ambayo inahusu taswira za dhahani za kiimani. Pale anaposema "Unibebe uniweze kwa nguvu zake Manani" mwimbaji huyu ana maana kwamba hata mapenzi yanataka Baraka kutoka kwa Mungu ili yaweze kufanikiwa. Hii inatokana na imani kwamba Mwenyezi Mungu ndie mwenye kutia nguvu juu ya kila kitu.

Vile vile, taswira ya kiteolojia ambayo inasawiri muktadha ya imani imetumika katika wimbo wa *Nimemridhi* pale Khadija Kopa anapotumia taswira ya "mizungu." Kama ilivyoelezwa hapo kabla kwamba hili ni neno lenye maana ya kutumia uchawi

au nguvu za majini ili kufanikisha jambo fulani. Kwa kutumia taswira hii tunapatiwa picha ya mizimu kama ifuatavyo:

> Kwa ridhaa yangu nimeridhia wala si **mizungu**
> Ni chaguo langu nimemchagua yumo moyoni mwangu
> Sitaki majunguu mlonipikia waja walimwengu…

Katika ubeti huo, neno "mizungu" lina maana ya nguvu za kishirikiana ambazo hupingwa na imani za kidini. Ili kusawiri picha hiyo, Khadija Kopa anakana kwamba mapenzi aliyonayo kamwe hayakuambatana na nguvu za mizimu. Vile vile, katika wimbo wa *Nimeridhi* Khadija Kopa anatumia taswira za "Majini," "Mungu" na "Jalali" ili kuakisi miktadha ya imani. Matumizi haya ya taswira yanajidhihirisha katika beti zifuatayo:

> **Majini** mizunguo mliyonuiaa muamuzi **Mungu**
> Mapenzi ni raha hayana hirinzi siyaamini
> Nimeridhia nae kaniridhi lawamazanini
> Nampenda kweli  kwake sijiwezi oo ya salaa
>
> Kashifa sijali nalienzi penzi vumbi ladhimu
> Nampenda kweli kwake sijiwezi oo by sweety
> Kashfa sijali nalienzi penzi oo ya habiby
>
> Bure kwenu ndoli mnajipa kazi ya kumwaga sumu
> Bure kwenu ndoli mnajipa kazi ya kumwaga sumu
> Namuomba **Jalali** atatuhifadhi mapenzi ya dongoo
> Naamini **Jalali** atatuhifadhi mapenzi ya dongoo

Katika beti za hapo juu, tunaona namna Khadija Kopa anavyosukumwa na miktadha ya imani katika kutumia baadhi ya taswira zake. Katika beti za hapo juu, taswira ya "majini" imetumika kuonesha kuwa hayana nguvu mbele ya Mungu. Aidha, katika beti hizo kuna matumizi ya taswira "Mungu" na "Jalali." Taswira hizi zinatupatia picha kwamba Mwenyezi Mungu ndie mwenye uwezo wa kuyalinda mapenzi yao.

Pia katika wimbo wa *Niliwaze* kuna taswira ya "hirizi." Dhana ya hirizi pia inaweza kuekwa katika miktadha ya imani aliyonayo mtu juu ya suala hilo. Mutiso (2012) anaieleza hirizi kuwa hutengenezwa kutokana na mawe, majani, mbegu, pembe, kucha, nywele, meno, madini, viwakilishi vya maumbo ya mwanadamu, medali, senti, na kadhalika. Anaendelea kueleza kuwa hirizi inaaminika kuleta baraka, kulinda na kutibu. Kwa mtazamo huu Khadija Kopa anaamini hirinzi hivi:

> Mapenzi ni raha hayana **hirizi** siyaamini
> Nimemridhi nae kaniridhi lawama za nini

Katika dondoo hilo, mtunzi anapoelza "Mapenzi ni raha hayana *hirizi* siyaamini" analenga kupingana na imani iliyomo miongoni mwa wanajamii kuwa hirizi huweza kutumika kufanikisha jambo fulani. Mawazo haya ya Khadija Kopa yanayojidhihirisha katika dondoo hilo yanapingana na yale ya Mutiso (2012) ambaye anaeleza kuwa hirizi hutumiwa kufanikisha baadhi ya mambo katika jamii. Kwa imani ya Khadija Kopa ni kwamba mapenzi hayawezi kufanikishwa kwa kutumia hirizi.

Kwa kutumia Msimbo wa Ki-seme ambao unahusiana na jinsi msomaji atakavyoishia kuipata picha ya mhusika fulani wa kifasihi, utafiti umebaini kuwa Khadija Kopa anajenga taswira inayosawiri uwezo wa Mungu juu ya kila kitu. Kwa kutumia uwezo huo, hata majini na hirizi huwa hazina nafasi katika kusaidia mapenzi.

### 4.3.5 Miktadha ya Kifasihi

Fasihi ni sanaa inayotumia lugha ili kufikisha ujumbe kwa jamii. Otieno (2017) anaeleza kuwa mtunzi wa kazi za fasihi huibua matarajio ya mpokeaji wa kauli

husika kwa kutumia vidokezo vinavyomvutia mpokeaji huyo na kuteka makini yake kwenye zile jumbe zilizomuhimu kwake ili kung`amua makusudio ya msemaji husika kwa kutumia lugha iliyofumbwa. Nyimbo ni moja kati ya utanzu wa fasihi simulizi, hivyo kama zilivyo tanzu nyengine nyimbo hutumia lugha ya kisanaa ikiwemo taswira ili kusawiri miktadha ya kifasihi. Hivyo data zilizokusanywa kutoka nyimbo teule za Khadija Kopa zimetumia taswira kusawiri miktadha ya sanaa ya fasihi. Kwa mfano, katika wimbo wa Mwanamke Mambo, mtunzi anatumia taswira zinazolenga kuonesha ujuzi wa kukitumia Kiswahili ili kuelezea ujumbe wake kama inavyojidhihirisha katika ubeti ufuatao:

Mwalilia wivu nimepata kitu bomba mie
Kazi kwenu wachovu sasa mambo yangu laivu mie
**Mtoto** bado nalipa na ngoma za uhakika
**Mtoto** naserebuka namwagia mahaba mie
Nna mkuna nyayoni maraha mpaka kichwani
Sasa mwalilia wivu nimepata kitu bomba mie
Zingatia mafundisho bibi alonifundisha

Katika wimbo huo, taswira ya "mtoto," imetumiwa na muimbaji kuonesha kwamba bado yuko katika rika la vijana na hivyo anaweza kuvutia mbele ya wanaume ndio maana anasema "Mtoto bado nalipa na ngoma za uhakika." Matumizi haya ya taswira yanaibua hisia za msikilizaji zinazosawiriwa na ujuzi wa lugha ya kifasihi. Mvuto wa vionjo hivyo vya lugha ya kifasihi unawafanya wapenzi wa nyimbo za taarabu kuvutiwa na nyimbo za Khadija Kopa. Mfano mwengine wa taswira inayosawiri muktadha wa kifasihi umetumika katika wimbo wa *Mwanamke Mambo* kama ubeti unaofuata unavyolithibitisha hilo:

Chumbani ukimfungia
Nitamuinda kama **paka**
Nitamuinda kama paka

Dirishani nitamtoa
Sitishwi nikitishika
Raha zimenikolea
Sitishwi nikitishika
Raha zimenikolea
Paka change paka

Katika dondoo hilo, “paka” ni taswira ya kizuolojia ambayo ina maana ya “kitu kinachokera.” Mwimbaji anatumia mbinu ya tashibiha ili kutujengea taswira hii pale anaposema “Nitamuinda kama paka,” anafananisha na mtu anapomtafuta paka ambaye tayari ameharibu. Uteuzi huu wa taswira unaweza kubainishwa kama mtindo mahususi wa Khadija katika kuiumba kazi yake. Kama asemavyo Jilala (2016) kwamba mwanafasihi huweza kuteua maneno maalumu ili kusawiri kile anachokikusudia ambapo uteuzi huo huwa ni aina moja wapo ya mtindo wa mwandishi wa fasihi.

Aidha, katika wimbo wa *Niliwaze* kuna matumizi ya taswira ya “vibati” inayosawiri muktadha wa kifasihi pale msanii anaposema “mpige vibati” ambayo inatupatia picha ya kueleza na kupigia kelele jambo fulani kwa lengo la kudhoofisha. Taswira hii inajitokeza hivi:

Maneno mseme mpige **vibati** hata mkizua
Na mtu hajanie baya halifiki mnajisumbuaa
Na mtu hajanie baya halifiki mnajisumbuaa
Nataka mseme penzi halitawaa

Taswira ya “kupiga vibati” imetumika ili kuibua mbinu ya kifasihi ya kumfanya msikilizaji asikie kitendo kinachozungumziwa. Kutokana na taswira hii msikilizaji anaweza kupata picha ya namna maaadui wa mapenzi yanayozungumziwa walivyokusudia kuharibu uhusiano huo wa mapenzi kati ya wapendanao. Kwa

kutumia nadharia ya Simiotikia katika msimbo wa Kiishara mtafiti amebaini kuwa Khadija Kopa amekuwa akitumia taswira kwa lengo la kuonesha usanii wa nyimbo hizo huku akifikisha ujumbe wake kwa jamii.

## 4.4 Athari za Matumizi ya Taswira Katika Nyimbo za Khadija Kopa

Lengo mahususi la tatu la utafiti huu likuwa ni kutathmini athari za kutumia taswira katika nyimbo za mahaba za Khadija Kopa. Mtafiti alizikusanya data na kuzitalii kwa mbinu ya usomaji makini na kugundua kwamba matumizi ya taswira katika nyimbo za mwimbaji huyo zina atahari chanya na hasi. Hivyo basi, katika sehemu hii mtafiti amewasilisha na kuchambua data zinazoonesha athari za matumizi hayo ya taswira katika nyimbo teule. Kwanza, utafiti umeonesha athari chanya za matumizi ya taswira hizo na baadaye kuwasilisha na kuchambua data zinaoonesha athari hasi za matumizi ya taswira hizo.

### 4.4.1 Athari Chanya za Matumizi ya Taswira katika Nyimbo za Khadija Kopa

#### 4.4.1.1 Kukuza Lugha

Kwa mujibu wa Taasisi ya Ukuzaji Mitaala (1988) wanaeleza kuwa lugha ni utaratibu wa kuwasiliana kwa kutumia maneno. Ingawa binaadamu anauwezo wa kuwasiliana kwa kutumia ishara kama vile mbinja, kutikisha kichwa nakadhalika lakini njia hizo hatuziiti lugha. Matumizi ya maneno hutegemea miktadha mahususi. Kutokana na ukweli huo, data zilizokusanywa na mtafiti zinaonesha kuwa matumizi ya taswira katika nyimbo teule za Khadija Kopa yamekuwa ni njia moja ya kukuza lugha ya Kiswahili. Hili linaweza kuthibitika kwa kutumia taswira ya neno “ngoma” katika wimbo wa *Mwanamke Mambo* kama linavyojidhihirisha katika ubeti ufuatao:

Ee mwanamke raha **ngoma** namtikisia
Unaenda sijigonge gonge nitakuvua weyee
Tutakula kwa matonge sambamba tutatumia
Ukiumwa kajigonge weye
Ukiumwa kajigonge weye

Ilielezwa hapo kabla kwamba BAKIZA (2010) wanalifasiri neno “ngoma” kuwa ni kifaa cha muziki ambacho kinawambwa kwa ngozi. Hata hivyo, taswira hiyo inapotumika katika mshororo “Ee mwanamke raha ngoma namtikisia” neno hilo linapata maana nyengine tofauti na ile iliyozoeleka. Maana hii ni “mwili” au “kiuno.” Wakati wa kuiimba nyimbo hiyo Khadija Kopa amekuwa akitingisha mwili wake ikiwa ni pamoja na kiuno ili kuonesha sadfa ya kile anachokizungumzia. Vile vile katika wimbo huo huo wa Mwanamke Mambo tunamuona namna mwimbaji teule anavyotumia taswira ya “buzi” ikiwa na maana ya “kumvuta mwanamme kufanya mapenzi ili kujipatia pesa.” Matumizi haya ya maneo yanajidhihirisha kama ifuatavyo:

Kwa mfano, katika wimbo wa *Mwanamke Mambo* kuna taswira “buzi.” Taswira hii inatupatia picha ya wanawake kufanya ngono holela. Hivyo taswira hii inaelezwa hivi:

Lipi anataka msaada na bwana kamkataa
Mke mwenza akiregea regea chuna chuna **buzi**
Ukiona mambo hayawezi kula kula vitu

Katika ubeti huu neno buzi limetumika likikengeusha maana ya kamusi iliyozoeleka ambayo inaelezwa na BAKIZA (2010) kwamba ni mnyama wa kufugwa mwenye ukubwa kama vile kondoo mwenye pembe zenye kuchoma, au ni kifaa cha nyumbani kinachotumika kukunia nazi. Hata hivyo, Khadija Kopa anaposema “Mke mwenza akiregea regea chuna chuna buzi” neno “buzi” lina kengeushwa maana hizo hapo juu

na kuwa na maana ya "kumchukua mwanamme na kufanya naye mapenzi." Kwa ujumla taswira zinazojengwa katika nyimbo teule ni kiungo muhimu cha kukuza lugha. Kwa kutumia msimbo wa Kiishara unaopatikana katika nadhatia ya Simiotiki mtafiti amebaini kuwa taswira hizo zimesawiri uhalisia wa namna jamii inavyotumia maneno kuzalisha maana za ziada ambazo huweza kutumika katika miktadha tofauti tofauti.

#### 4.4.1.2 Kuendeleza Utamaduni

Vile vile, data zilizokusanywa kutoka nyimbo za taarabu za Khadija Kopa zinaonesha kuwa matumizi ya taswira yametumika kutokana na miiko ya utamaduni wa jamii iliyomkuza. Ni jadi ya Waswahili kutozungumza lugha inayohusu maingiliano ya kimwili wazi wazi. Ili kutii miiko hiyo wanajamii wamekuwa wakitumia njia ya lugha isiyo ya moja kwa moja. Hili linathibitika katika ubeti ufuatao unaoonekana katika wimbo wa *Mwanamke Mambo*:

Eee mwanamke raha ngoma namtikisia
Kalipasua **fenesi** ee kalipasua
Kalipasua fenesi ee kalipasua
Kalipasua fenesi ee kalipasua

Katika ubeti huo, taswira ya "fenesi" bila shaka imetumika kusawiri "kiungo cha maingiliano ya kimwili cha mwanamke." Hata hivyo, katika jamii ya Uswahilini utamaduni hauruhusu kueleza viungo hivyo waziwazi. Kuhusu suala la matumizi ya mafumbo ikiwemo taswira kama kipengele cha kulinda miiko ya utamaduni, Beck (2005) anadai kuwa masuala yasiyoruhusiwa kuzungumzwa waziwazi miongoni mwa Waswahili huwasilishwa kutumia mafumbo. Mawazo haya yanalandana na yale ya Otieno (2017) ambapo katika utafiti wa nyimbo za taarabu aligundua kuwa kuna baadhi ya masuala ya kijamii ambayo hayafai kuwekwa wazi kwa sababu aina

Kwanza kabisa, baadhi ya msukumo wa kuficha maana kusudiwa miongoni mwa watunzi wa taarab hutokana na utamaduni wa jamii, kwa hivyo, ili kukuza matumizi ya lugha ya heshima kizazi baada ya kizazi hutumia mafumbo. Mawazo haya yanafanana na yale Khamis (2002) anayeeleza kuwa nyimbo za taarab huangazia masuala ya wanajamii kwa lugha ya mafumbo. Hali hii inaambatana na mila na desturi za Waswahili zinazomzuia kutamka masuala fulani hadharani. Kwa kutumia msimbo wa Kiurejelezi wa nadharia ya Simiotiki mtafiti amebaini kuwa taswira zinazotumika katika nyimbo za Khadija Kopa zinalengo la kutozungumzia masuala ya uhusiano wa mapenzi kwa njia ya wazi.

#### 4.4.1.3 Kukuza Fasihi

Athari nyengine ya taswira katika nyimbo za Khadija Kopa ni ile ya kuonesha sanaa ya fasihi katika jamii. Taarabu ni kipera kinachopatikana katika utanzu wa ushairi na taswira ndio uti wa mgongo katika ushairi. Kutokana na hali hiyo ndio maana mtunzi huyu amekuwa akitumia taswira ili kusawiri ujumbe aliokusudia kwa jamii kwa mbinu ya fasihi. Matumizi haya ya taswira ili kukidhi miktadha ya kifasihi yanajidhihirisha katika wimbo wa *Mwanamke mambo* kama ifuatavyo:

> Mwalilia wivu nimepata kitu bomba mie
> Kazi kwenu wachovu sasa mambo yangu laivu mie
> **Mtoto** bado nalipa na ngoma za uhakika
> **Mtoto** naserebuka namwagia mahaba mie
> Nna mkuna nyayoni maraha mpaka kichwani
> Sasa mwalilia wivu nimepata kitu bomba mie
> Zingatia mafundisho bibi alonifundisha

Katika wimbo huo, taswira ya “mtoto,” inayopatikana katika mshororo unaoeleza“Mtoto bado nalipa na ngoma za uhakika,” imejengwa ili kuakisi uzuri wa

mazungumzo yaliyomo katika fani ya fasihi. Mfano mwengine wa taswira inayotumiwa ili kuakisi fani hii ya fasihi ni kutokana na matumizi ya taswira ya neno "bibi," kama inavyojidhihirisha katika wimbo wa *Mwanamke Mambo* kama inavyojidhihirisha katika ubeti ufuatao:

Ukiumwa kajigonge weye
Nyumba utaniachia
Simtoi hata chembe
Chepeto mchepeto
Umemchagua weye
Hutokula hutokula **bibi** peke yako

Katika wimbo huo, taswira ya "bibi" kama inavyojidhihirisha pale Khadija Kopa anaposema "Hutokula hutokula bibi peke yako" anatupatia taswira ya kuelewa kuwa mzungumzaji anamuambia mwanamke mwenzake. Hata hivyo, badala ya kutumia maneno Aidha, katika wimbo huo kuna matumizi ya taswira ya "paka" kama inavyojidhihirisha katika ubeti ufuatao:

Chumbani ukimfungia
Nitamuinda kama **paka**
Nitamuinda kama paka
Dirishani nitamtoa
Sitishwi nikitishika
Raha zimenikolea
Sitishwi nikitishika

Katika dondoo hilo, taswira ya paka kama inavyojidhihirisha pale mwimbaji anaposema "Nitamuinda kama paka," inalenga kuonesha namna mwimbaji atavyofanya juhudi ili kumtafuta na kumpata mpenzi anayemtaka. Hata hivyo, kwa sababu hii ni fasi mtunzi imetumika taswiri iliyojengwa katika tashibiha ya namna msanii atakavyomtafuta mpenzi wake kama paka. Kwa ujumla fasihi hutumika

wahusika kama vile watu, wanyama, mazimwi, majini ili kusanii lakini ujumbe unaotolewa unahusu binadamu. .

Vile vile, Khadija Kopa ametumia taswira za vitu vya kawaida kama sehemu ya kipengele cha fani katika fasihi. Kwa kutumia taswira za vitu vya kawaida kitu kimoja hukiwakilisha kitu chengine matokeo yake ni kwamba ile sifa ya fasihi inapatikana. Kwa mfano, katika wimbo *Niliwaze*, kuna matumizi ya taswira ya "njia." Taswira hii inajidhihirisha hivi:

Nipendeze niliwaze ili niwe furahani
Nitulize nipendeze penzi penzi liwe na imani
Mafisadi tuwabeze washindwe pita **njiani**
Aaa mafisadi tuwabeze washindwe pita **njiani**
Unibebe uniweze kwa nguvu zake manani

Katika dondoo hilo, tunapatiwa taswira ya "Mafisadi tuwabeze washindwe pita *njiani*." Katika mshororo huu tunachokibaini ni kwamba mtunzi ametumia maneno teule ili kujenga mvuto kwa hadhira yake. Kutokana na mvuto huo ndio anaakisi ile maana halisi ya maana ya fasihi ambayo inalengo la kuibua uzuri na mvuto kwa kutumia maneno. Kwa kutumia nadhria ya Simiotiki kwenye msimbo wa Kiishara tunaona kuwa matumizi ya ishara hutumiwa na Khadija Kopa katika nyimbo zake zikiwa na lengo la kuibua mvuto wa kifasihi huku zikifikisha ujumbe alioukusudia kwa jamii.

Matumizi haya ya taswira yanalandana na nadharia ya Simiotiki katika msimbo wa Kiishara. Taswira zilizotumika katika nyimbo hizo ni ishara ambazo zinaonesh anamna Khadija Kopa alivyo na ujuzi katika utunzi wa kazi za fasihi. Ndio maana

amekuwa akitumia maneno yaliyozoeleka kutumika katika jamii na kuyatumia ili kujenga taswira zake na hatimae kufumbata ujumbe aliokusudia kwa fumbo la fasihi.

#### 4.4.1.4 Kutambulisha Uwezo wa Mungu

Pamoja na athari zilizokwishajadiliwa hapo juu, data zilizokusanywa zimeonesha kuwa Khadija Kopa anatumia nyimbo kama mojawapo ya njia ya kutambulisha uwezo alionao Mwenyezi Mungu ambao hauwezi kushindwa na kitu chochote. Hii imebainika kutokana na kutumia baadhi ya maneno ambayo yanatoa taswira ambayo huifanya hadhira ibaini muelekeo alionao Khadija Kopa kuhusu suala la imani inayofungamana na dini. Hili linadhihirika katika wimbo wa *Nimeridhi* katika beti zifuatazo:

**Majini** mizunguo mliyonuiaa muamuzi **Mungu**
Mapenzi ni raha hayana hirinzi siyaramlini
Nimemridhi nae kaniridhi lawama zanini
Nampenda kweli kwake sijiwezi oo ya salaa
Kashifa sijali nalienzi penzi vumbi ladhimu
Nampenda kweli kwake sijiwezi oo by sweety
Kashfa sijali nalienzi penzi oo ya habiby

Bure kwenu ndoli mnajipa kazi ya kumwaga sumu
Bure kwenu ndoli mnajipa kazi ya kumwaga sumu
Namuomba **Jalali** atatuhifadhi mapenzi ya dongoo
Naamini **Jalali** atatuhifadhi mapenzi ya dongoo

Matumizi ya taswira za maneno "Mungu," "Jalali" na "Majini" ni taswira ambazo zinatubainishia imani aliyonayo Khadija Kopa kuhusu uhusiano wa Mungu na mwanadamu. Kwa kutumia maneno "Jalali" na "Mungu" ambayo ni visawe vya neno Mwenyezi Mungu yaani muumba mbingu na ardhi na viliomo ndani yake Khadija Kopa anajitambulisha kuwa ni muuimini wa dini ya Uislamu, hasa hasa kwa kutumia neno "Jalili" ambalo linatokana na lugha ya Kiarabu. Kutokana na imani ya

kidini aliyonayo, anaamini kwamba majini ni viumbe ambavyo navyo hutegemea kwa Mungu hivyo kamwe hawawezi kuwa na nafasi yoyote katika mapenzi yake mbele ya nguvu za Mungu. Athari hii ya utambulisho kama inavyojidhihirisha katika nyimbo teule za Khadija Kopa linalandana na mawazo ya Fairclough (1989) anavyosema maneno hubeba itikadi za jamii. Hivyo nyimbo hizo zinaonesha itikadi ya imani ya dini aliyonayo msanii huyu. Kwa kutumia nadharria ya Simiotiki mtafiti amebaini kuwa matumizi ya taswira Mungu na Jalali yanasawiri msimbo wa Kiishara wa nadharia hiyo. Kutokana na ishara hizo mtafiti anapata ujumbe unaohusu uwezo wa Mungu katika kubariki mapenzi ya mwimbaji huyo.

#### 4.4.1.5 Kuifunza Jamii

Moja ya kazi ya fasihi ni kuifunza jamii katika nyanja mbalimbali za maisha ya jamii (Mulokozi, 1996). Nyimbo za taarab kama mojawapo ya kipera cha fasihi hutumika kuifunza jamii. Hivyo athari nyengine ya nyimbo za Khadija Kopa ni kuifunza jamii iliyomzunguka. Kwa mfano, katika wimbo wa Full Stop jamii inafundishwa kujiepusha na ngono holela kama inavyojidhihirisha katika beti ifuatayo:

Mtoto wangu wa kiume nisikilizeni
Mnaojiita **masharobaro** nisikilizeni
Nyie mabarobaro nisikilizeni
Nawambia kina kaka wanawake wanajua
Pale panapo utamu wamepapamba maua
Ukikosa gonoria Ukimwi utakuuwa
Ukimwi utakuuwa
Ukimwi utakuuwa
Eee usiguse **moto** utakuunguza
Eee usiguse **moto** utakuunguza

Katika beti hii kuna matumizi ya taswira ya “masharobaro” inayotupatia picha ya vijana wakisasa ambao wamekuwa na tabia ya kuishi maisha ya anasa na hata kufanya ngono holela. Kutokana na tabia hiyo, katika wimbo huo kunatumiwa taswira ya “moto” ikiwa na maana ya kufanya ngono holela. Kitendo hicho kinaathari kubwa kwa afya yao ikiwa ni pamoja na kupata maambukizo ya magonjwa kama vile Ukimwi na gono. Tunachojifunza hapa ni kwamba maradhi kama vile Ukimwi huambukizwa kwa njia kuu ya maingiliano ya mwili hasa yanayotokana na ngono holela ambayo vijana wengi hupendelea kama sehemu maisha yao ya anasa. Mafunzo mengine yanayopatikana katika nyimbo za Khadija Kopa ni pamoja na mbinu za kuweza kuendeleza uhusiano mzuri wa ndoa. Mbinu hizo zinafunzwa ndani ya wimbo wa *Mwanamke Mambo* kama ifuatavyo:

Mwanamke **kikuba**
Mwanamke **hina**
Mwanamke **udi**
Mimi namfukizia

Katika ubeti huo, kuna matumizi ya taswira “kikuba,” “hina” na “udi” yanayotupatia picha ya mapambo ya jadi anayopaswa kuyaendeleza mwanamke ili kuwa na mvuto kwa mwanamme walie kwenye uhusiano wa mapenzi. Funzo tunalolipata hapa ni kwamba katika kuendeleza uhusiano ulio mzuri na bora katika ndoa ni lazima wanawake kuhakikisha wanahakikisha wanaendeleza usafi. Kwa ujumla nyimbo za Khadija Kopa ni dafiana inayoifunza jamii yake. Mawazo haya yanaungana na yale ya Askew (2002) ambaye kwa maoni yake, nyimbo za taarab hutumia lugha ya kisanaa kwa wingi katika juhudi za watribu kumulika masuala hasa ya kijamii. Anaendelea kudai kuwa japo nyimbo za taarab huonekana kuangazia masuala ya mapenzi katika kauli zinazoanguliwa, ndani yake huwa na maana fiche ambapo

masuala ya kijamii, kisiasa, mijadala ya kijinsia na utambulisho huonyeshwa kwa kufumba. Vile vile, kwa kutumia msimbo wa Kiurejelezi wa nadharia ya Simiotiki mtafiti amebaini kuwa taswira katika nyimbo za Khadija Kopa zinaihusu jamii yake.

### 4.4.2 Athari Hasi za Taswira katika Nyimbo za Taarab za Khadija Kopa

Kwa upande mwengine utafiti umebaini kuwa yapo matumizi ya taswira katika nyimbo za Khadija Kopa ambayo yana athari hasi kwa hadhira na jamii kwa ujumla. Katika utafiti huu athari hasi zinamaana ya mambo ambayo ama hayawezi kukubalika na wanajamii kama sehemu ya utamaduni au huwa yanatatiza katika kupata ujumbe uliokusudiwa. Kwa muktadha huo athari hasi katika nyimbo hizo zimejidhihirisha kama ifuatavyo:

#### 4.4.2.1 Kuhamasisha Ngono Holela

Maingiliano ya mwili kwa ujumla huwa hayakubaliki miongoni mwa jamii ya Waswahili ispokuwa yale yaliyohalalishwa kwa misingi ya dini. Pamoja na miiko hiyo iliyomo katika jamii data zilizokusanywa na mtafiti zinaonekana kuna matumizi ya taswira katika nyimbo za Khadija Kopa ambazo undani wake unaonesha kukengeusha miiko hiyo ya utamaduni. Kwa mfano, katika wimbo wa Mwanamke Mambo tunapata taswira ya "buzi" pale msanii huyo anaposema "Mke mwenza akiregea regea chuna chuna **buzi.**" Taswira inayopatikana hapa ni kwamba mwanamke huyo anahamasishwa kuvanya uzinzi kwa kishingizio cha kwamba mke mwenza amelegea. Kama inavyotambulika kwamba katika jamii ya Tanzania neno buzi ni msimu ambao unamaana ya mwanamme ambaye anafanya mapenzi na mwanamke asiyekuwa mke wake wa ndoa ambapo mwanamke huyo lengo lake kuu

ni kujipatia kipato. Kwa ujumla mafunzo kama haya hayawezi kukubalika miongoni mwa wanajamii.

#### 4.4.2.2 Kuendeleza Mwanamke Kuwa Chombo cha Starehe cha Mwanamme

Njogu na Chimerah (1999) wanaieleza nafasi ya mwanamke katika jamii kwa kutumia dhana ya "umenke." Hii ni nafasi ambayo imekuwa ikijadiliwa na wanajamii ikiwemo wanafasihi pamoja na wahakiki wa kazi za fasihi. Kwa sababu hiyo Khadija Kopa amekuwa akitumia taswira katika nyimbo zake ili kujadili nafasi ya mwanamke katika jamii. Kwa mfano, katika wimbo wa *Mwanamke Mambo* kunataswira ambazo zinasawiri nafasi ya mwanamke katika jamii kama ifuatavyo:

> Mwanamke **kikuba**
> Mwanamke **hina**
> Mwanamke **udi**
> Mimi namfukizia

Katika ubeti huo, kuna matumizi ya taswira "kikuba," "hina" na "udi" yanayotupatia picha ya mapambo ya jadi anayopaswa kuyaendeleza mwanamke kwa lengo la kumridhisha mwanamme. Picha inayopatikana katika taswira hizi ni kwamba Khadija Kopa analengo la kutoa mafunzo yanayomtaka mwamke kujipamba ili aweze kuridhiwa na mwanamme. Matokeo yake ni kwamba mwanamke anakuwa si kitu cha thamani iwapo hatoridhiwa na mwanamme. Aidjha, katika wimbo wa Nimeridhi taswira ya "Mtoto" inatumiwa na msanii ambapo inajitokeza kama ifuatavyo:

> **Mtoto** bado nalipa na ngoma za uhakika
> **Mtoto** naserebuka namwagia mahaba mie
> Nna mkuna nyayoni maraha mpaka kichwani
> Sasa mwalilia wivu nimepata kitu bomba mie

Katika dondoo hilo, taswira ya “Mtoto naserebuka namwagia mahaba mie,” inaonesha namna mwanamke yeye mwenyewe alivyokubali kuwa chombo cha starehe mbele ya mwanamme. Baadhi ya wahakiki kama vile Mulokozi (1999) wanaonesha kuwa kitendo cha mwanamke kujilazimisha kumridhisha mwanamme kimapenzi ni ukandamizaji wa mawanmke. Mawazo haya yanaungwa mkono na Zaja (2008) ambaye anasema kuwa wanawake katika jamii wamenyimwa nafasi ya kumiliki mali na kujitegemea hivyo basi ili kujikimu kimaisha sharti wamtegemee mwanamume. Mwanamume amepewa hadhi ya juu katika jamii na ndio maana anang’anganiwa na wanawake kwa kuwa anaonekana kama mwenye suluhisho la mahitaji wa wanawake. Mawazo haya yanayokosolewa na wahakiki hawa ndiyo tunayokutana nayo tusikilizapo nyimbo za Khadija Kopa.

### 4.4.2.3 Matumizi ya lugha ya Matusi

Haya ni matumizi ya lugha ambayo huwa haikubaliki katika jamii kutokana na kukiuka miiko ya jamii. Data zilizokusanywa na mtafiti zimnaonesha kuwa Khadija Kopa amekuwa akitumia taswira ili kuepuka kuzungumzia masuala yanayohusu maingiliano ya kimwili kati ya mwanamme na mwanamke. Ili kulifanikisha hilo anajaribu kutumia taswira katika nyimbo zake lakini taswira hizo bado zimekuwa mazoea. Tunaposema kuwa taswira inamaana kuwa baadhi ya taswira hizo zimezoeleka kiasi ambacho zinaonekana kama ni matumizi ya lugha ya kawaida. Kwa mfano, katika wimbo wa *Mwanamke Mambo* hali hii inajitokeza kama ifuatavyo:

Ee mwanamke raha **ngoma** namtikisia
Unaenda sijigonge gonge nitakuvua weyee
Tutakula kwa matonge sambamba tutatumia
Ukiumwa kajigonge weye
Ukiumwa kajigonge weye

Katika ubeti huo, kuna matumizi ya taswira inayojengwa kwenye neno “ngoma,” ambalo linatupatia picha ya mwili pale linapotumika katika “Ee mwanamke raha ngoma namtikisia.” Matumizi haya ya taswira katika miktadha ya beti hii yanatupatia picha ya lugha ya matusi kutokana na kusawiri harakati za tendo la kufanya ngono. Neno ngoma limezoeleka mno katika jamii ya Waswahili kutumika katika harakati za mapenzi hivyo pamoja na kwamba neno hilo limetumika kama taswira yenye kuficha maana lakini limekuwa na mapungufu yake lutokana umazoea huo katika jamii. Matokeo yake ni kwamba jamii inajikuta ikidharau ama kuchukia baadhhi ya nyimbo hizo za taarabu kwa madai kwamba zinaeleza matusi wazi wazi. Hii yote huwa inachagizwa na mtindo wa sasa uliozikumba nyimbo za taarab. Mawazo haya yanashadidiwa na Barker (1999) na Khamis (2004) wanaoeleza kuwa ipo haja ya kudumisha mtindo wa zamani wa utunzi wa taarab ili kuepuka athari hasi za kigeni ambazo huenda zikadidororesha maadili ya jamii ya Waswahili.

#### 4.4.2.4 Kuchochea Migogoro

Vile vile, taswira katika nyimbo za Khadija Kopa zinaweza kusababisha migogoro miongoni mwa wanajamii. Mathalani, katika wimbo wa *Mwanamke Mambo* kuna matumizi ya taswira ya “golira,” na “mkorogo” ambazo kwa ujumla zimetumika zikiwa na lengo la kukejeli wanawake wengine. Taswira hizo zinajidhihirisha kama ifuatavyo:

Jicho mwanangu halooo
Jicho mwanangu halooo
Sio wewe ulokunuka
Shepu ya **golira** chapwaa
Mie Beautiful
Beautiful natural
Sio mkorogo ulojipaka
Sio mkorogo ulojipaka

Katika dondoo hilo hapo juu yataswira ya neno "golira" ambayo inatupatia picha ya wanyama wa jamii ya kima wanafananishwa na umbo la binadamu pale mwimbaji anaposema "Shepu ya golira chapwa." Matumizi haya ya lugha huweza kuibuwa migogoro miongoni mwa wahusika kutokana na kufananishwa na mnyama. Vile vile, matumizi ya taswira iliyomo kwenye neno "mkorogo" yenye maana ya "rangi ya ngozi iliyochubuliwa kutokana na vipodozi ili kupata ngozi nyekundu" inalengo la kuwakejeli wale wenye kutumia vipodozi hivyo na kwamba kutokana na kuondoa umbile lao la asili kunawafanya hawana thamani mbele ya wanaume.

## 4.5 Hitimisho

Sura hii imeangazia kwa kina uwasilishaji na uchanganuzi wa data kuhusu aina za taswira katika nyimbo za Khadija Kopa. Sehemu ya pili inaeleza miktadha inayomsukuma Khadija Kopa kutumia taswira katika nyimbo zake za taarabu na mwisho, sehemu hii imewasilisha athari za matumizi ya taswira katika nyimbo teule. Imebainika kuwa kuna athari chanya na athari hasi za kutumia taswira katika nyimbo za Khadija Kopa kama ilivyoelezwa katika sura hii. Hivyo, kukamilika kwa uwasilishaji na uchambuzi wa data umetoa fursa ya kuonesha majibu ya maswali ya utafiti huu.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inaonesha muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu.Katika sura hii majibu ya maswali ya utafiti huu yanapatikana kwa muhtasari. Kimsingi sura hii inabainisha namna malengo ya utafiti huu yalivyokamilika kwa mutawalia. Hivyo basi, sura hii imejibainisha kama ifuatavyo:

## 5.2 Muhtasari wa Tasnifu

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kubainisha taswira zilizopo katika nyimbo za taarab za mahaba za Khadija Kopa na miktadha iliyopelekea kuibuka kwa taswira hizo pamoja na athari zake kwa jamii. Ili kulifikia lengo hilo, mtafiti alichagua nyimbo tano mahaba za Khadija Kopa ambazo zinamatumizi ya taswira. Kutokana na msingi huo utafiti huu uliziteua nyimbo tano ambazo ni *Niliwaze*, *Nimemridhi*, *Mwanamke Mambo*, *I Love You* na *Full Stop*.

Utafiti huu ulikuwa na malengo mahususi matatu ambapo lengo mahususi la kwanza lilikuwa ni; Kubainisha taswira katika nyimbo za taarab za Khadija Kopa. Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo; “Kuna aina ngapi za taswira katika nyimbo za taarab za Khadija Kopa?” Lengo mahususi la pili lilikuwa ni “Kubainisha miktadhainayosababisha Khadija Kopa kutumia taswira hizo katika nyimbo zake.”Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo “Ni miktadha ipi iliyopelekea ubunifu wa taswira katika nyimbo za tarabu za Khadija Kopa?” Na lengo mahususi la tatu lilikuwa ni “Kuchunguza athari za taswira hizo kwa jamii.”

Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo “Je, taswira hizo zina athari gani kwa jamii?”

Tasnifu hii ina jumla ya sura tano. Sura ya Kwanza ni sura ya utangulizi ambayo inaeleza mambo ya msingi ya utafiti huu. Sura hii imebainisha na kueleza usuli wa mada ya utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, lengo kuu na malengo mahususi, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na muundo wa tasnifu hii.

Sura ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa nadharia. Sura hii inasehemu ya utangulizi, dhana muhimu katika utafiti huu ambazo ni utangulizi wa sura, dhana ya taarab, taswira na aina za taswira, mapitio ya maandiko kuhusu nyimbo. Aidha, sura hiyo inabainisha pengo la utafiti huu. Mwisho sura imeeleza nadharia ya Simiotikia ambayo imeongoza utafiti huu. Mwisho sura imetoa hitimisho.

Sura ya tatu ya tasnifu hii imeelezea mbinu na vifaa vilivyotumika kukusanya data za utafiti huu. Vipengele vilivyojumuishwa katika sura hii ni usanifu wa utafiti, eneo la utafiti na walengwa wa utafiti. Vipengele vyengine vilivyooneshwa ni sampuli na mbinu za usampulishaji. Aidha, sura hii inaelezea mchakato wa ukusanyaji wa data na uthabiti na kuaminika kwa data na maadili ya utafiti.

Sura ya nne imefanya uchambuzi na uwasilishaji wa data za utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu ndogo ndogo tatu. Sehemu hizo zimepangwa kutegemea malengo ya utafiti huu. Sehemu ya kwanza imewasilisha na kuchambua data zihusuzo aina za taswira katika nyimbo za kimahaba za Khadija Kopa. Sehemu ya pili ni uwasilishaji na uchambuzi wa data zinazohusu miktadha iliyosababisha

Khadija Kopa kutumia taswira hizo katika nyimbo zake, na sehemu ya mwisho imebainisha athari chanya na hasi za matumizi hayo ya taswira katika jamii. Mwisho, sura imetoa hitimisho.

Sura ya tano imehitimisha kwa kutoa muhutasari wa utafiti, matokeo ya utafiti na mapendekezo. Sura hii inaeleza kwa muhtasari kile kilichogunduliwa na mtafiti. Maswali yaliyoongoza utafiti huu yanaelezwa majibu yake kwa ufupi kama ilivyobainika kupitia uwasilishaji na uchambuzi wa data katika sura ya nne ya tasnifu hii. Hivyo basi, matokeo ya utafiti huu yalikuwa kama ifuatavyo:

## 5.3 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na malengo matatu. Hivyo uchambuzi wa data umetoa matokeo kama ifuatavyo:

### 5.3.1 Lengo Mahususi la Kwanza

Lengo mahsusi la kwanza la Utafiti huu lilikuwa ni: Kubainisha taswira katika nyimbo za Khadija Kopa. Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti la kwanza lisemalo: “Ni aina ngapi za taswira katika nyimbo za Khadija Kopa?”

Matokeo ya utafiti huu yalionesha kuwa nyimbo za Khadija Kopa zimekuwa zikitumia taswira za kizuolojia, taswira za botania, taswira za kiastromia, taswira za kijiolojia, taswira ya kiteolojia na taswira za vitu vya kawaida.

### 5.3.2 Lengo Mahsusi la Pili

Lengo mahsusi la pili la utafiti huu lilikuwa ni: “Kubainisha miktadha inayosababisha Khadija Kopa kutumia taswira hizo katika nyimbo zake.” Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo “Ni miktadha ipi iliyopelekea ubunifu wa

taswira katika nyimbo za taarab za Khadija Kopa? Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa miktadha inayosababisha ubunifu wa taswira katika nyimbo za Khadija Kopa ni miktadha ya mapenzi, miktadha ya utamaduni, miktadha ya utandawazi, miktadha ya imani na miktadha ya kifasihi.

### 5.3.3 Lengo Mahsusi la Tatu

Lengo mahsusi la tatu la utafiti huu lilikuwa ni: "Kuchunguuza athari ya taswira hizo kwa jamii." Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo "Je, taswira hizo zina athari gani kwa jamii?" Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa taswira katika nyimbo za Khadija Kopa zina athari chanya na hasi katika jamii. Athari chanya ni pamoja na kukuza lugha, kuendeleza utamaduni, kukuza fasihi, kutambulisha na kuifunza jamii. Kwa upande mwngine taswira hizo zina athari hasi ambazo ni kuhamasisha ngono holela, kuendeleza mawazo ya kumfanya mwanamke kuwa chombo cha starehe kwa mwanamme, kutumia lugha ya matusi na kuchochea migogoro.

## 5.4 Hitimisho

Utafiti huu ulilenga kuchunguza taswira katika nyimbo za taarab za mahaba za Khadija Kopa. Kwa ujumla mtafiti aligundua kuwa nyimbo za mahaba za Khadija Kopa zimekuwa zikitumia taswira ili kusawiri miktadha ya mapenzi, utamaduni, imani, utandawazi na miktadha ya ubunifu wa kifasihi. Matumizi haya ya taswira huwa na atahari chanya na hasi katika jamii.

## 5.5 Mapendekezo

Utafiti huu unapendekeza kama ifuatavyo:

### 5.5.1 Mapendekezo kwa Watafiti Wengine

Utafiti huu ulijikita kuchunguza taswira katika nyimbo za mahaba za Khadija Kopa. Hivyo ni wazi kwamba bado ipo nafasi ya kufanya tafiti nyengine katika nyimbo za taarab zikiwa na malengo tofauti na utafiti huu kama vile kuchunguza majigambo ya waimbaji wa nyimbo za taarab hasa za wanawake akiwemo Khadija Kopa. Pia, ipo haja ya kuchunguza namna waimbaji wa taarab wanavyoendeleza ukandamizaji wa mwanamke katika nyimbo zao.

### 5.5.2 Mapendekezo kwa Wasanii wa Nyimbo za Taarab

Utafiti huu unapendekeza kuwa waimbaji wakiwemo waimbaji wa taarab watumie taswira zilizokuwa hazikuzoeleka katika jamii ili kulinda miiko ya utamaduni inayowataka watu kutoeleza masuala yahusuyo maingiliano ya kimwili wazi wazi.

### 5.5.3 Mapendekezo kwa Jamii

Utafiti unapendekeza kuwa jamii inapaswa kufuata dhamira zinazoelezwa na Khadija Kopa ili kuendeleza usatawi ulio bora katika maisha ya kila siku.

## MAREJELEO

Abdalla, A R. (2018). *Kuchunguza Dhamira na Fani katika Nyimbo za Taarab Asilia: Mifano ya Nyimbo za Shakila Said Khamis.*Tasnifu ya MA-Kiswahili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

Adungo, C. (2019). *Gwiji wa Taarab: Khadija Kopa.* Imepakuliwa leo tarehe 3/4/2020 kutoka

Ali, H. S. (2005). *Mafumbo Yanayopatikana katika Nyimbo za Harusi katika Ndowa za* Unguja. Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

Babbie, E. (1999). The *Basics of Social Research.*.Belmont: Wardsworlth Publishing Company. Barthens, R. (1994). *The Simiotic Challenges*. Califonia: Barkey University Press.

Beyanga, A. (2004). *Taswira ya Ngombe katika Nyimbo za Harusi za Jamii ya Washubi* Tasnifu ya Uzamili. Dar es Salaam, Chuo Kikuu Cha Dar-es-Salaam.

Cohen, L. M. and Keith, M. (2000). *Research Methods in Education (5th edition)* London: Routledge Publishers

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. London: Oxford University Press

Gionga, N. W. (2017). Uchambuzi Linganishi wa Fani na Maudhui ya Nyimbo za Harusi za Kimeru na za Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili MA-Kiswahili katika Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Khamis, A.W (2016). *Kuchunguza Dhamira za Nyimbo za Siti Bint Saad*. Tasnifu ya MA-Kiswahili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

Khamis, S. N. (2017). *Mabadiliko katika Nyimbo za Taarab na Uwasilishaji Wake Kulingana na Wakati.* Tasnifu ya MA-Kiswahili Chuo Kikuu cha Dodoma.

Khatib, M. S. (1992). *Taarab Zanzibar*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Khatib,Muhammed (2011).*Chanjo za Matakwa ya mwanamume katika mwili wa mwanamke Ulinganisho wa Muyaka Bin Haji na Shaaban Robert*.Tasnifu ya shahada ya Uzamifu Haijachapishwa.Chuo Kikuu cha Dodoma.

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International Publishing Ltd. (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age nternational Publishing Ltd.

Mohamed, A. R. (2015). *Kuchunguza Dhima za Nyimbo za Ngoma ya Msondo wa Pemba.* Tasnifu ya Uzamili ya MA-Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mohamed, O. S. (2018). *Usasa wa Mashairi ya Nyimbo za Taarab ya Sasa: Fani na Maudhu.* Tasnifu ya Uzamivu Katika Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

Mzee, A. F. (2011). Athari za Nyimbo za taarab ya Mipasho kwa Jamii ya Wazanzibar. Dodoma: Chuo Kikuu Cha Dodoma.

Mulokozi, M. M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam:

Mulokozi (1996), Fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Muhammed, O. S. (2010). *Mchango wa Nyimbo za Unyango katika Kumkomaza Mwari Kinyumba.* Ripoti Mintarafu Wilaya ya Kinondoni nchini Tanzania. Chuo Kikuu cha Kiislam Uganda.. Kampala, Uganda.

Muhando, P. na Balysidya, N. (1976). *Fasihi na Sanaa za Maonyesho*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mungai, M.J. (2014). Fani katika Nyimbo Teule za Anastacia Mukabwa. Tasnifu ya Uzamili MA Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi.

Njeri, M. J. (2016). *Mwingiliano Tanzu katika Mdern Taarab-Mipasho*. Tasnifu ya Uzamivu ya Chuo Kikuu cha Moi.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia Na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ndungo, C. W. na Mwai, W. (1991). *Kiswahili Studies: Part Two*. Nairobi: University of Nairobi.

Otieno, O. J. (2017*). Uchanganuzi wa Kipragmatiki wa Sitiari katika Nyimbo za Taarab: Mfano wa Mzee Yssuf na Mwanahawa Ally- Unguja.* MA-Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es Salam.

Rajab, F H (2016) *Kuchunguza chanjo za mapenzi katika nyimo za taarabu za Seif Salim, Chuo Kikuu Huria Tanzania Tasnifu Haijachapishwa*.

Rashid, H. U. (2013). *Mafunzo ya Nyimbo za Jando na Unyago kwa Jamii ya Wahiyao wa Masasi ya Lulindi.* Tasnifu ya Uzamili ya MA- Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Sengo, T. S. Y. (1973*). Dhima ya Fasihi kwa Maendeleo ya Jamii.* Jarida la Kiswahili. Dar-es Salaam: TUKI.

Sengo, T. S. Y. (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi*. Dar es Salaam: AKADEMIA.

Simiyu, F. W. (2011). *Kitovu cha Fasihi Simulizi.* Nairobi: Serengeti Educational Publishers Ltd.

Senkoro, F. E. M..K . (1987). *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre. TAKILUKI, (1983). *Fasihi Simulizi ya Zanzibar.* Dar-es-salaam: Tanzania Publishing house.

Taufiq, B. (2016). Taswira Katika Ushairi wa Mwinyi Hatibu: Kutoka Malenga wa Mrima Nimerudi. Tasnifu ya MA-Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

Wamtila, K. W. (2002). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Nairobi: Kenya Oxford University Press. (2003*). Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia.* Chuo Kikuu Dar-es-Salam. (2008). *Kanzi za Fasihi Msingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vde- Muwa Publishers Limited.

Waziri, M. M. (2016). *Kuchunguza Dhima za Nyimbo za Singo katika Kijiji cha Uzini Zanzibar*. Tasnifua ya Uzamili MA-Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Yego, E. K. (2013). *Nafasi ya Mwanamke: Jinsi Inavyotetewa katika Nyimbo za Taarab za Zanzibar*. Tasnifu ya MA-Kiswahili Chuo Kikuu cha Nairobi.

## KIAMBATANISHO

### Na. 1: Nyimbo za Taarab za Mahaba za Khadija Kopa

- **NILIWAZE**

Nipendeze niliwaze ili niwe furahani

Nitulize nipendeze penzi liwe na imani

Mafisadi tuwabeze washindwe pita njiani

Aaa mafisadi tuwabeze washindwe pita njiani

Unibebe uniweze kwa nguvu zake manani

Niamini nijitangaze iwepo vikaoni

Unibebe uniweze kwa nguvu zake manani

Niamini nijitangaze iwepo vikaoni.

KIITIKIO

Nipende kwa raha kila ailaa

Nitaje kwa hiari nilacho uwe hunaaa

Nitaje kwa hiari nilacho uwe hunaaa

Penzi nimekukubali bila hofu naomba

Kwako mimi sina hali hao walotuandama

Penzi lako kwangu mali wendacho uwe hunaa.

Penzi linataka malezi sote kuaminiana

Pasiwe na kizuizi washindwe la kutukana

Penzi  lataka malezi sote kuaminiana

Tuzidishe ujuzi washindwe na kutukana

Na mimi nitakuenzi kwa marefu na mapana

Ooo na mimi nitakuenzi kwa marefu na mapana

Penzi  liote mizizi raha zilizofanana

Lisiwe na kizuizi mtuone twapendana.

KIITIKIO

Nipende kwa raha kila ailaii

Nitaje kwa hiari nilonacho uwe hunaa

Nitaje kwa hiari nilonacho uwe hunaa

Nami nimekukabidhi hakika ovu lawamaa

Pemzi langu ulienzi hao walotuandamaa

Nipende nikumbatie kifuani uniweke

Wa wivu na waumie na nyuma tusigeuke

Wa wivu na waumie na nyuma tusigeuke

Mapenzi tupalilie tuyarambe tusichoke

Aaa mapenzi tupalilie tuyarambe tusichoke

Nipende nifurahie wabaya waadhirike

Rohoni na waumie tuwagune tuwacheke

KIITIKIO

Nipende kwa rahaa

Nami nimekukabidhi  hakika ovu lawama

Nakupenda ntakuenzi  hawana tuandama

Na nitakupa mapenzi uwe nacho uwe huna

- **NIMEMRIDHI**

Kwa ridhaa yangu nimemridhia wala si mizungu

Ni chaguo langu nimemchagua yumo moyoni mwangu

Sitaki majunguu mlonipikia waja walimwengu

Majini mizungoo mliyonuiaa muamuzi mungu

Mapenzi ni raha hayana hirinzi siyaramlini

Nimeridhia nae kaniridhi lawama za nini

Nimemridhi mwenyewe

Awe wake awe wangu

Ndio chaguo languu

Ooo mpenzi ni hali malii

Ooo mpenzi ni hali malii

Simuachi kamwe nimemthibiti mti mtekewa

Maneno mseme mpige vibati hata mkizua

Na mtu hajame baya halifiki mnajisumbuaa

Na mtu hajame baya halifiki mnajisumbuaa

Nataka mseme mpe atiati

Penzi halilawaa

Nimemridhi mwenyewe awe wake awe wangu

Awe wanguu ndio chaguo languu

Ooo mpenzi ni hali malii

Ooo mpenzi ni hali malii

Nampenda kweli  kwake sijiwezi oo ya salaa

Kashifa sijali nalienzi penzi vumbi ladhimu

Nampenda kweli kwake sijiwezi oo by sweety

Kashfa sijali nalienzi penzi oo ya habiby

Bure kwenu ndoli mnajipa kazi ya kumwaga sumu

Bure kwenu ndoli mnajipa kazi ya kumwaga sumu

Namuomba jalali atatuhifadhi mapenzi ya dongoo

Naamini jalali atatuhifadhi mapenzi ya dongoo

Nimemridhi mwenyewe awe wake awe wangu

Awe wanguu

Ndio chaguo languu

Ooo mpenzi  ni hali malii

Ooo mpenzi  ni hali malii

Waaja msinisakame bure kwa sababu ya mpenzi

Waaja msinisakame bure kwa sababu ya mpenzi

Niache ning'are niacheni nifure wee

Sitaki maudhi

Mwalilia wivu nimepata kitu bomba mie

Kazi kwenu wachovu sasa mambo yangu  laivu mie

Mtoto bado nalipa na ngoma za uhakika

Mtoto naserebuka namwagia mahaba mie

Nna mkona nyayoni maraha mpaka kichwani

Sasa mwalilia wivu nimepata kitu bomba mie

Zingatia mafundisho bibi alonifundisha

- **MWANAMKE MAMBO**

Nimeshachimba mati itakutoka

Nimeshafunga utamu kaupata

Tutakwenda sambamba

Ukidaka tadaka

Nitakutoa ushamba hataki nimemtenga

Kama wewe mwenye nyumba ona mie kanitaka ooo kanitaka

Kanitaka mwenyewe kanitaka

Nishamsomba nishamsomba nishamchukua

Ooo majambo nachichitia

Oo majambo eee nachichitia

Kwa mavitu ameroa kwako hakupendelea

Kwa mavitu ameroa hakutaki kanambia

Nampa kitumbua mafuta hujirambia

Nampa kitumbua mafuta hujirambia

Wala sitombania nampa kisawa sawa

Wala sitombania nampa kisawa sawa

**KIITIKIO**

Eee mwanamke mambo

Eee mwanamke jicho

Ee mwanamke mambo

Ee mwanamke raha ngoma namtikisia

Unaenda sijigonge gonge mbio nitakujivua weyee

Tutakula kwa matonge sambamba tutatumia

Ukiumwa kajinyonge weye

Ukiumwa kajinyonge weye

Nyumba utaniachia

Simtoi hata chembe

Chepeto mchepeto

Umemchengua

Chepeto mchepeto

Umemchengua

Hutokula hutokula bibi peke yako

Hutokula hutokula peke yako

Ooo sambasamba ee tutachambua

Ooo sambasamba mie ee tutachambua

Eee tutachambua

Ni wako akiwa kwako akitoka naopoa

Ni wako akiwa kwako akitoka naopoa

Ni wako akiwa kwako akitoka naopoa

Ni wako akiwa kwako akitoka naopoa

Naramba mpaka ukoko

Hoi kachanganyikiwa dali

Naramba mpaka ukoko

Hoi kachanganyikiwa

Hakuna cha peke yako

Ukichukua ntachukuaa

Hakuna cha peke yako

Ukichukua ntachukuaa

KIITIKIO

Eee mwanamke mambo

Eee mwanamke jicho

Ee mwanamke mambo

Ee mwanamke raha ngoma namtikisia

Unaenda sijigonge gonge mbio nitakujivua weyee

Tutakula kwa matonge sambamba tutatumia

Ukiumwa kajigonge weye

Ukiumwa kajigonge weye

Nyumba utaniachia

Simtoi hata chembe

Chepeto mchepeto

Umemchengua

Chepeto mchepeto

Umemchengua

Kitatimka kivumbi

Kivumbi kitatimka kivumbi

Chumbani kimfungia

Chumbani kimfungia

Chumbani kimfungia

Chumbani kimfungia

Nitamuinda kama paka

Nitamuinda kama paka

Dirishani tamtoa

Sitishwi nikatishika

Raha zimenikolea

Sitishwi nikitishika

Raha zimenikolea

Paka cha kupaka  dada

Out nimekutoa

Mwanamke kikuba

Mwanamke hina

Mwanamke udi

Mimi namfukizia

Mwanamke kikuba

Mwanamke hina

Mwanamke udi

Haiba nnaijua

KIITIKIO

Eee mwanamke mambo

Eee mwanamke jicho

Eee mwanamke mambo

Eee mwanamke raha ngoma namtikisia

Hongera hongera mumeo msobe msobe

Mimi sina papara mimi  sina papara

Kwako wewe mimi haleni

Ooo kisamkore ngoma nimeichukua

Alikutaka kwa kwa bahati mbaya

Baileti lee

Baileti lee

Usishindane na mimi

Mimi ni mzuri

Na utamu nnao

Na utamu nnao

Na utamu nnao

Jicho mwanangu halooo

Jicho mwanangu halooo

Sio wewe ulokuruka

Shepu ya golira chapwaa

Mie  Beautiful

Beautiful natural

Sio mkorogo ulojipaka

Sio mkorogo ulojipaka

Mpira ukiruswa nadaka

Mpira ukiruswa nadaka

Nafunga goli kwa tintaka

Karibu tapewa talaka

Mpira ukiruswa nadaka

Mpira ukiruswa nadaka

Nafunga goli kwa tintaka

Karibu tapewa talaka

Jitazame ujimurike jitazame

Jitazame ujimurike jitazame

Ngurwa ngurwa kichwa boya

Ngurwa ngurwa kichwa boya

Una umbile la kike halipoteya maboya

Una umbilea la kike halipoteya maboya

Tuliza boli usitirike asije kushtukia

Tuliza boli usitirike asije kushtukia

Mie ndiye kitu chake maoja kasehelea mpenzi

Mie ndie kitu chake kasaheleaa

Mwanamke masal mumeo kamfanyia

Mwanamke liwa mimi namsugua

Mwanamke masal mumeo kamfanyia

Mwanamke liwa mimi namsugua

Mwanamke liwa mimi namsugua

Eee mwanamke mambo

Eee mwanamke jicho

Eee mwanamke mambo

Eee mwanamke raha ngoma namtikisia

Kalipasua fenesi ee kalipasua

Kalipasua fenesi ee kalipasua

Kalipasua fenesi ee kalipasua

Lipi anataka msadaa na bwana kamkataa

Lipi anataka msadaa na bwana kamkataa

Mke mwenza akiregea regea chuna chuna buzi

Ukiona mambo hayawezi kula kula vitu

Ukiona kafunga funga kaza buti

Mpira ukirushwa nadaka

Mpira ukirushwa nadaka

Nafunga goli kwa tintaka

Karibu tapewa talaka

- ***I LOVE YOU***

Kukupenda nilazimu

Wewe wangu natamka

Wasikutie wazimu hakuna

Nilomtaka

Na mimi sikulaumu

Kupendwa ndo nataka

Nia yangu yalazimu

Sisemi siri naweka

Sisemi siri naweka

Mwenye akili timamu

Basi yamefahamika

Penzi hili lako tamu

Kwa yule nnomtaka

mwenye akili timamu

basi yamefahamika

penzi hili lako tamu

mpenzi nnakutaka

Penzi hili maalum kwa yule ninomtaka

mpenzi kuwa timamu

namba yako hiishika

penzi hili maalum kwa yule ninomtaka

mpenzi sikudhulumu

namba yako hii shikaaa

*I love you baby*

*I love you baby*

*I love you baby*

*I love you baby*

Tutulie ili tuwaoneshe

Washuhudie ili wapate kasheshe

Tutulie ili tuwaoneshe

Washuhudie ili wapate kasheshe

Nakupenda kweli kweli

Nakuzimikia kweli

Nakupenda kweli kweli

Nakuzimikia kweli

*I love you*

*I love you*

*I love you*

*I love you*

*I mis you*

*I mis you*

*I mis you*

*Forever and ever*

Mkinidharau nimewasahau

Wataka tibika zidisha dau

Mkinidharau nimewasahau

Wataka tibika zidisha dau

Mkinidharau nimewasahau

Wataka tibika zidisha dau

Usihofu mpenzi wangu

Na yao tuwadharau

Usijali baby wangu

Na yao tuyasahau

Tupendane tupendane

Hadi yauumul-kiama

Tupendane tupendane

Hadi mwisho wa dunia

- ***FULL STOP*** **KHADIJA KOPA**

Ili wapate tabu kwa mara nyengine tena

Mimi ni mtu wa watu nisojuwa kunong’ona

Jamani mapaparazi najuta kuniona

Mnaingilia mapenzi tunayopeana na bwana

Nikianza na mizizi penzi si la mwaka janaa oooo

Hatukuingia juzi juzi aaa jiji la Dar-es-salam

Tumelifanyia kazi tukashusha na vilima

Tumeyafika mapenzi joto joto lazizima

Atakae jitia bazazii ajue hana usalama

Nitamfugia kazii na mji  atauhama

Nitamfugia kazii na mji  atauhama

Mustafu wote kimya supa Issa kigori naongea

Mustafu acheni kelele kazi ruhsa kujitetea

Mustafu wote kimya supa Issa kigori naongea

Mustafu acheni kelele kazi ruhsa kujitetea

Ole wenu mnaopitaaa njia za panya kunifatilia

Mimi ni komando wa kike ala ala ntawaripua

Ole wenu mnaopitaaa njia za panya kunifatilia

Mimi ni komando wa kike ala ala ntawaripua

Tena nnalipa bishoti wa ukwee na nnajua kudengua

Kanipenda kanizimikia kweli na hasa pale nnaporembua

Tena nnalipa bishoti wa ukwee na nnajua kudengua

Kanipenda kanizimikia kweli na hasa pale nnaporembua

Sasa wezi wa mabwana nawaambia ntawachakachua

Nawapa onyo fuli stop ili chalenji fulgiaa

Sasa wezi wa mabwana nawaambia ntawachakachua

Nawapa onyo fuli stop ili chalenji fulgiaa

Nyie taipu zenu za vichochoroni

Ndizo zinzowafaa

Sio wangu mimi chumba na varanda tena ghorofani nampandia

Sio wangu mimi chumba na varanda tena ghorofani nampandia

Mustafu jipangene upya hapa kwangu mmechemka

Nna ladha tamu sanaa ooo ndio mana hataki kutoka

Hata mje na waganga lori zima himaya yangu kashafiika

Mlilie mizimu na makafara

Na mchinje hata paka

Mustafu jipangene upya hapa kwangu mmechemka

Nna ladha tamu sanaa ooo ndio mana hataki kutoka

Hata mje na waganga lori zima himaya yangu kashafiika

Mlilie mizimu na makafara

Na mchinje hata paka

Ala wajifanya unalipa

Hutafuti wako ukamweka

Wewe huwezi milki yangu

Baby quti wa kiafrika

Kwanza mie niko peke yangu

Nimetulia sina shaka

Nimetulia na mume wangu

Mtoto wa uhakika

Ala wajifanya  unalipa

Hutafuti wako ukamweka

Mimi huwezi milki yangu

Baby quti  wa kiafrika

Kwanza mimi niko peke yangu

Nimetulia sina shaka

Nimetulia na mume wangu

Mtoto wa uhakika

Vikarolaiti  vyenu vinavyowapa jeuri Hivyo

Vikarolaiti vyenu tavipiga marufuku hapa

Mimi nina rangi yangu

Sitaki uso wa vibaka

Mimi nna rangi yangu na kopa bado nalipa

Bandika bandika mimi nabandua

Mjini maarifa huna unalolijua

Bandika bandika mimi nabandua

Tumependana wawili weeoe umejichopeka

Hakutaki  pesa mbili hujijui taka taka

Bandika bandika mimi nabandua

Bandika bandika mimi nabandua

Tumependana wenyewe

Maneno maneno ya nini

Eti zere nyote boe

Kwani mnataka nini

Sasa nnawambia

Kijana yuko makini

Wala hahitaji kocha

Nafsimwe yuko chini

Hahitaji msaada wa jezi

Kiwanja anacho ndani

Anavyotua akipaa kama guko Marekani

Kama yuko marekani ooo

Kama yuko marekani

Eee usiguse moto utakuunguza

Eee usiguse moto utakuunguza

Napajua hapa bongo pameenea vituko

Nakujua kule zenji kumeenea vituko

Nakujua Mombasa mjini pameenea vituko

Kinadada wakwambia mambo ni mpambaiko

Kama hujajipodoa hapa bongo huna soko

Hapa bongo huna soko

Hapa bongo huna soko

Bila ya asumini na udi kule zenji huna soko

Bila kueka kikuba na Mombasa huna soko

Ee usiguse moto utakuunguza

Ee usiguse moto utakuunguza

Na kina dada wa bongo kwa kweli wajanja sana

Kina dada wa Mombasa na nyie wajanja sana

Na kina dada wa zenji kwa kweli wajanja sana

Mkifika uwanjani macho mnatazamana

Sasa mkitoka nje mnagombea mabwana

Sasa mkitoka nje mnagombea mabwana

Eee usiguse moto utakuunguza

Eee usiguse moto utakuunguza

Wapenzi wangu nawapenda msifikirini utani

I love you so much msifikiri utani

Nimewamiss msifikirini utani

Wapenzi wangu nawapenda msifikirini utani

Hasa mnapochezaga mnaposimama stejini

Na pale mnapopagawa mnapokuwa uwanjani

Ungekuwa embe dodo ningewala na majani

Nengawala na majani

Nengawala na majani

Eee usiguse moto utakuunguza

Eee usiguse moto utakuunguza

Mtoto wangu wa kiume nisikilizeni

Mnaojuta masharobaro nisikilizeni

Nyie mabarobaro nisikilizeni

Nawambia kina kaka wanawake wanajua

Pale panapo utamu wamepapamba maua

Ukikosa gonoria ukimwi utakuuwa

Ukimwi utakuuwa

Ukimwi utakuuwa

Eee usiguse moto utakuunguza

Eee usiguse moto utakuunguza

Tooti motoo watu wote

Tooti motoo mpisha nipite

Tooti mpango  mzimaa

Tooti mpango  mzimaa

Tooti mpango  mzimaa

Tooti mpango  mzimaa

Loliondo kwa babu

Sharobaro kapewa kikombe

Akasema nangoja mrijameni

Loliondo kwa babu

Sharobaro kapewa kikombe

Akasema nangoja mrijamen